

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Tano – Tarehe 14 Aprili, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Shirika la Viwango Tanzania kwa Mwaka 2005/2006 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania Bureau of Standards (TBS) for the Year 2005/2006)*.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 54

**Uchomaji Moto Ovyo Mimitu**

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria ya *Local Government* ya mwaka 1982 na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 zinatoa madaraka makubwa kwa Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji kusimamia na kudhibiti masuala yote ya mazingira katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kupiga marufuku uchomaji wa moto ovyo katika mapori na mimitu pamoja na maagizo ya Viongozi Kitaifa; na kwa kuwa pamoja na madaraka hayo sehemu nyingi hapa nchini huchomwa moto ovyo hasa nyakati za kiangazi bila hatua yoyote kuchukuliwa:-

(a) Je, ni mkoa gani Tanzania unaoongoza kwa uchomaji ovyo mimitu na mapori?

(b) Kwa kuwa uchomaji moto wa maeneo umeathiri sana uoto wa asili katika nchi yetu; ni mikakati ipi endelevu ya Halmashauri za Wilaya imewekwa ili kudhibiti uchomaji ovyo misitu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; ninadhani swali hili lilikwenda mahali kusiko.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ninapenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, sehemu nyingi katika nchi yetu, huchomwa moto ovyo hususan nyakati za kiangazi na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira, ikiwa ni pamoja na upotevu wa bayoanuwai nyingi ya misitu. Aidha, uchomaji hovyoy misitu umechangia kwa kiasi kikubwa katika kuenea kwa hali ya jangwa na ukame nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikoa yote yenye misitu aina ya miyombo, inayo matukio mengi ya myoto. Mikoa hiyo ni Rukwa, Mbeya, Tabora, Kigoma, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Morogoro pamoja na Pwani. Kwa kuwa, moto unavuka mipaka ya mikoa bila kujali ulianzia wapi na ni vigumu kubaini mkoa gani unaongoza kwa uchomaji moto katika Tanzania.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji, kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, imeandaa na inaendeleza mikakati ambayo inalenga kudhibiti uchomaji moto kama ifuatavyo:-

Uelimishaji wa jamii kupitia vyombo vya habari kuhusu madhara ya moto na tahadhari zinazotakiwa kuchukuliwa ili moto usitokee. Aidha, Wizara ya Maliasili na Utalii inaandaa na kutoa mada katika kipindi maalum cha “Misitu ni Uhai” kinachoandaliwa na kutangazwa na Shirika la Habari Tanzania kila wiki ili kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kulinda misitu dhidi ya moto. Uelimishwaji wa jamii, hufanywa pia kwa njia ya *video* na machapisho kama vile kalenda, vipeperushi, mabango na stika. Bango maarufu litwalo “Kilio cha Mti” huchapwa na kusambazwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kila mwaka kupitia kanda saba za misitu. Kanda hizo zikiwa ni pamoja na Kibaha, Kigoma, Songea, Moshi, Dodoma, Shinyanga na Mbeya. Vilevile vibao vinavyosomeka “Usichome Moto”, hubandikwa katika misitu ya hifadhi ili kuikumbusha jamii kuchukua tahadhari ya kuchoma moto katika misitu hii.

Njia nyingine ni ushirikishwaji wa jamii katika kuhifadhi na kuendeleza misitu unaofanywa. Wananchi wanahimizwa kuhifadhi na kuendeleza misitu kwa njia ya usimamizi shirikishi wa misitu kama ilivyoielezwa katika Sera ya Taifa ya Misitu. Aidha, jamii imeelekezwa kutenga misitu katika maeneo yao na kuhifadhi kama misitu ya hifadhi ya vijiji. Vilevile wananchi wanashirikishwa katika kulinda na kuendeleza misitu ya Serikali iliyohifadhiwa kwa njia ya ubia. Hadi sasa jumla ya hekta milioni tatu zipo chini ya usimamizi shirikishi katika Wilaya 57 hapa nchini. Imedhihirika kwamba, matukio ya moto katika misitu inayolindwa kwa njia ya usimamizi shirikishi yamepungua. Mfano mzuri ni Mkoa wa Shinyanga, ambako matukio ya moto katika misitu yamepungua kwa kiasi kikubwa. Hali hii inatokana na jamii kumilikishwa misitu iitwayo “ngitiri” ambayo huhifadhiwa na kulindwa kwa njia za jadi.

Njia ya tatu, vijiji vingi hapa nchini tayari vina sheria ndogondogo kuhusu udhibiti na uchomaji moto. Vijiji vingine vipo kwenye mchakato wa kuandaa na kufanya mapitio ya sheria ndogondogo ili kuendana na wakati. Kwa mfano, baadhi ya vijiji vya Mkoa wa Singida; mhalifu wa uchomaji moto anatakiwa kulipa mbuzi kwa kila hekari, pamoja na gharama nyingine ambazo zimewekwa na kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Cynthia Ngoye, kwa jitihada zake za utunzaji wa mazingira, sio tu katika Mkoa wa Mbeya, bali Tanzania kwa ujumla.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cynthia Ngoye ni Mwenyekiti wa *NEMC*, kwa hiyo, inaeleweka. Mheshimiwa Ngoye, swali la nyongeza.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kama kawaida yake ni maarufu sana katika kujibu maswali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba, ili kudhibiti hali ya uharibifu wa mazingira hapa nchini ni muhimu vilevile kuwa na sheria muhimu sana na madhubuti, ambazo zinasimamiwa vizuri huko vijijini. Yapo matatizo ambayo yamejitokeza kwamba, sheria hizi zinapokuwa zimeletwa huku ngazi ya kitaifa, hususan zile sheria mpya na hata zile zinazofanyiwa marekebisha, huchukua muda mrefu sana kurudishwa katika Halmashauri na Halmashauri nyingi sana zinalalamika. Je; Serikali ipo tayari kuwa na utaratibu mzuri sasa wa kuharakisha sheria hizi ziwe zinarudi haraka kwa Halmashauri ili ziweze kufanya kazi kama ambavyo sheria zetu tunazozitunga hapa sasa hivi zinavyoharakishwa kurudishwa? Hilo swali la kwanza.

Swali la pili; imejitokeza kwamba mara nyingi hizi sababu za uchomaji wa moto wa mapori zinatokana na kutokuwa na elimu kiasi ambacho hufanya wananchi wengi wajishirikishe katika uwindaji wa vinyama vidogovidogo kwa kuchoma moto, hasa hasa katika Mikoa ya Rukwa na vilevile katika Mikoa ya Morogoro wanawinda vinyama vidogovidogo bila kutumia njia za kisasa. Je, Serikali ipo tayari sasa kutoa elimu ya

kutosha kwa hawa wawindaji ili wawe wanatumia njia za kisasa katika kuwinda wanyama badala ya kuchoma mapori?

**NAIBU SPIKA:** Maswali ya nyongeza yalikuwa marefu mno, Mheshimiwa Waziri majibu?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwa hivi sasa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ina kitengo maalum ambacho kinapitia *by-laws* zote kwa haraka ili ziende kwa Waziri mwenye dhamana kuzihakiki na pia kuzisaini, tayari kwa kuzirudisha kwenye halmashauri. Kwa hiyo, kwa hivi sasa tumejiimarisha sana katika Wizara yetu kuhakikisha kwamba, hizi sheria ndogondogo za aina yoyote ambazo zinatoka katika Halmashauri, zinapitiwa kwa haraka na zinarudishwa kwa walengwa kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za uchomaji moto ziko nyingi; kuna sababu za uwindaji kama alivyosema, kuna sababu za kimila, kuna sababu za kilimo, sababu za uzembe tu na adhalika. tu anatupa sigara kwenya msitu, moto unawaka. engine kwa jili ya kilimo, kama ndugu angu wa Pwani; anapalilia ile mikoroshu kwa kuchoma. Ndugu angu wa Morogoro wanapalilia migomba kwa kuchoma. Kwa hiyo, hizi ni sababu nyingi ambazo zinasababisha uchomaji wa misitu. Kwa wale wawindaji wadogowadogo kama nilivyosema, tumewapa madaraka wanakijiji.

Kwa hiyo, tunatoa elimu kuanzia ngazi ya kijiji, ndio maana kuna sheria ndogondogo ambazo zimetungwa ili kudhibiti hali hiyo. Nina uhakika elimu ya kutosha ikizidi kutolewa, watu watabadilika na baadaye kwa kuangalia athari za mazingira, wananchi wataelimika na kudhibiti myoto isiwe inatokea mara kwa mara.

**NAIBU SPIKA:** Swali hili limechukua muda mrefu, kwa hiyo, tunaendelea na yanayofuata. Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha.

Na. 55

**Maombi ya Kusaidia Mpango wa Kuboresha  
Mazingira Wilayani Siha**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu Wananchi wa Wilaya ya Siha wameonyesha shauku kubwa ya kupanda miti katika maeneo ya makazi na katika vyanzo vya maji; na kwa kuwa wananchi hao walishaomba Serikali kusaidia mpango wa kuboresha mazingira na hata kutengeneza andiko:-

(a) Je, hatua gani zimefikiwa katika kutekeleza maombi hayo?

(b) Je, wakati maombi hayo yakiwa yanasubiriwa hakuna msaada wowote ule unaoweza kutolewa na Serikali ili kutekeleza Mpango wa Wilaya wa kupanda miti ipatayo 1,000,000 kila mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mbunge wa Siha, ninaomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda kuwapongeza Wananchi wa Wilaya ya Siha, wakiongozwa na Mbunge wao, kwa kuonyesha shauku kubwa ya kupanda miti katika maeneo ya makazi na katika vyanzo vya maji. Shauku hii na ari hii ya kupanda miti katika maeneo ya makazi na vyanzo vya maji, inaendana sambamba na utekelezaji wa mkakati wa kuhifadhi mazingira na ardhi na vyanzo vya maji nchini. Moja ya changamoto zinazobainishwa katika mkakati huu ni uharibifu wa mazingira utokanao na ukataji miti kwa ajili ya kuni, mkaa na ujenzi. Mkakati huu pia umebaini uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji kutokana na uvamizi wa wafugaji na shughuli za kilimo kwenye maeneo haya. Hivyo, hatua zilizopangwa kuchukuliwa na Wananchi wa Siha, zinalenga katika kukabiliana na moja ya changamoto zilizobainishwa katika mkakati nilioutaja hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Mwanri, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba, Wilaya ya Siha, ilileta maombi ya kugharimia Mpango wa Wilaya wa Kuboresha Mazingira. Baada ya kuupitia Mradi huu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, iliona kwamba, Mradi huu unaweza kufikiriwa kupata ufadhili chini ya Programu ya Miradi Midogomidogo ya Mfuko wa Mazingira Duniani, yaani *GEF Small Grant Program* au Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kupambana na Umasikini kupitia utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira. Hata hivyo, Mradi huu baada ya kupitiwa ulirudishwa kwa wahusika ili wauboreshe kulingana na miongozo iliyowekwa na uandaaji wa miradi inayofadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia au ile inayofadhiliwa na Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kupambana na Umasikini kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Kimataifa wa Mazingira. Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, inawasiliana na Programu ya Miradi Midogomidogo ya Mfuko wa Mazingira Duniani na washiriki wengine wa sekta ya mazingira ili kupata fedha za kuisaidia Halmashauri ya Siha kutekeleza Mradi huu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa Hifadhi ya Mazingira, kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009, imeanzisha kifungu nambari 261146 katika bajeti yake, kiitwacho *Environmental Management Service*, ambacho Wizara mbalimbali zinaweza kutenga fedha kwa ajili ya kuhifadhi mazingira kupitia kifungu

hiki. Halmashauri za Wilaya ni vyema zikatumia kifungu hiki katika kutenga fedha kwa ajili ya kutunza na kuboresha mazingira ikiwa ni pamoja na upandaji miti hususan katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapenda kumshukuru Mheshimiwa Mwanri, kwa juhudi zake katika kuboresha mazingira ya Wilaya ya Siha, Mkoa wa Kilimanjaro na Tanzania kwa ujumla.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Ninaomba nichukue nafasi hii, kwa niaba ya Wananchi wote wa Jimbo la Siha na Wilaya ya Siha, kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa hapa. Maombi haya ambayo aliletewa andiko katika Wizara hii ambayo iko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, yalipelekwa kwa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na bahati nzuri yumo humu ndani. Nilipeleka wakati nilipokuwa Mbunge mara ya kwanza, hii ni safari yangu ya pili kuwa Mbunge.

Ninaomba kujua hizo harakati ambazo anazizungumzia Naibu Waziri ni lini mtapata hayo majibu kwamba kazi hiyo itafanyika?

Pili, kwa vile ninajua kwamba Serikali ina majukumu makubwa na mengi; na kwamba inaweza ikachukua muda; kwa vile Wilaya ya Siha ni Wilaya mpya na changa, ambayo hata mafungu yake hayafiki kwa hivi sasa; je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuandaa *an ad-hock arrangement* kwa ajili ya Wilaya ya Siha ili niweze kwenda kupanda miti kama maelekezo yanavyotolewa Serikali? Ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mazingira wa Zamani, Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninakiri kwamba, ombi lake ni la muda mrefu kabisa na nilishiriki katika kutoa maelekezo ya jinsi ya kulishughulikia. Atuwie radhi kwamba, imechukua muda mrefu lakini mimi na yeye tumezungumza wiki iliyopita kuhusu hili suala na tukakubaliana kwamba, aniletee upya andiko kama lilivyo sasa ili niliweke katika nyongeza ya makabidhiano ya kazi na Mheshimiwa Waziri wa sasa wa Mazingira. Kwa hiyo, tutaliendeleza na ninajua kuna nafasi nyingi sana; si mradi mkubwa, tunatafuta kama shilingi milioni 60 na haiwezekani tukazikosa fedha za kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu hatua za dharura kama alivyojibiwa katika swali la msingi, tunamsihi kwamba, mambo haya yote yanaanzia katika Halmashauri. Kwa hiyo, Halmashauri ikitoa kipaumbele kwa hili suala, nina hakika ndani ya Serikali tunaweza tukatafuta njia ya kuisaidia, lakini haiwezi ikatoka juu ikaenda chini. Kwa hiyo, ninamwomba wapitishe azimio katika Halmashauri, halafu tutafute fedha kwa pamoja hata kama ni za dharura. Ahsante.

**Wavuvi Wadogo Wadogo - Zanzibar**

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID (K.n.y. MHE. FATMA ABDALLA TAMIM)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa wavuvi wadogo wadogo kutoka Zanzibar wanapokuwa katika shughuli za uvuvi hasa katika Kisiwa cha Mafia hutakiwa kukata tena leseni:-

Je, ni kwa nini wanatakiwa kukata tena leseni?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma abdalla Tamim, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za uvuvi kwa upande wa Tanzania Bara, husimamiwa na Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2005. Kwa kuwa suala la uvuvi si la Muungano, Leseni za Uvuvi zinazotolewa Zanzibar, hazitumiki Tanzania Bara na hivyo hivyo Leseni za Uvuvi zinazotolewa Tanzania Bara, hazitumiki Zanzibar, kwa sababu kila upande wa Jamhuri hutumia sheria yake ya uvuvi. Katika mgawanyo wa majukumu kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, leseni za vyombo vyenye urefu wa mita 11 kwenda chini, hutolewa na Halmashauri za Wilaya kwa upande wa Tanzania Bara. Sheria hiyo niliyoitaja kwa upande wa Tanzania Bara, ndiyo hutumika kuandaa sheria ndogondogo hizo katika ngazi ya Halmashauri na ninaamini sheria hizo ndogo hukidhi mahitaji katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kirefu, wavuvi wa Zanzibar ambao hutumia vyombo vya uvuvi vyenye urefu wa mita 11 kwenda chini, huja kuvua Tanzania Bara kwa utaratibu unaofahamika kama uvuvi wa dago. Hali kadhalika wavuvi kutoka Tanzania Bara, huenda kuvua Zanzibar kwa utaratibu huo huo. Kulingana na utaratibu tuliokubaliana kupitia Serikali zetu mbili, wavuvi wa dago kutoka Zanzibar hutakiwa kuonyesha leseni zao halali kutoka Zanzibar na barua ya utambulisho.

Afisa Uvuvi wa Halmashauri husika Tanzania Bara, hukagua na kuhakiki nyaraka hizo na kisha akiridhika hukagua idadi ya wavuvi, chombo, pamoja na zana za uvuvi zitakazotumika katika uvuvi unaokusudiwa na kuelekeza wavuvi sehemu za kufanyia uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utaratibu huo mzuri tuliojiwekea, wapo wavuvi wachache ambao hutaka kuvua nje ya utaratibu wa dago uliokubalika, ambao ni vipindi viwili vya miezi mitatu mitatu kwa mwaka. Wavuvi hao hutakiwa kutimiza

masharti ya sheria, yaani kukata leseni. Wavuvi wanaokaa muda mrefu zaidi ya ule uliokubalika, hulazimika kuwa na leseni za msimu unaofuata kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ya Zanzibar ili kuhakikisha kuwa, taratibu tulizokubaliana zinaeleweka kwa wavuvi wetu na ili kuhakikisha kuwa, uvuvi wa dago unaendeshwa bila usumbufu wala malalamiko na kuwawezesha wavuvi hao kupata kipato ili kukidhi mahitaji yao na kuwaondolea umaskini.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii, niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninamuuliza kama ifuatavyo:-

Wapo baadhi ya Maafisa wanatumia ubabe na wakati mwingine kuwatisha wavuvi au wakati mwingine hata kudai rushwa katika kuwakabili wavuvi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atatueleza wanachukua hatua gani katika kuwakabili maafisa kama hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa leseni ya chombo inakuwa ni rahisi kuliko leseni ya dago ya miezi mitatu; je, utaratibu huu hawauangalii tena ili kuhakikisha kuwa ili kuondoa yale manung'uniko ya wavuvi watoe leseni kubwa ya dago kuliko ya chombo chenye?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, lazima ijulikane kwamba, nchi yetu ni nchi ambayo inafuata Utawala Bora na wa Kisheria. Kwa hiyo, ndugu zetu wanapotoka Zanzibar kwa vyovyote vile, hawatakiwi kubabaishwa na Afisa yeyote mahali wanapoenda kuvua. Endapo wanapata matatizo, basi tutahakikisha kwamba sheria inachukua mkondo wake, lazima waje wavue kwa utaratibu na wasibughudhiwe kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu leseni kwamba zinatolewa mara mbili badala ya mara moja; ninafikiri mtu akishakata leseni kule Zanzibar, atakuwa ametumia fedha na kama anakuja miezi mitatu hatuna haja tena kusema lete fedha ukate leseni. Hata hivyo, tunahakikisha kwamba, vipindi vya miezi sita anaweza kuja kuvua akimaliza miezi mitatu anaenda anarudi ili mradi aje na zile nyaraka ambazo zinatakiwa.

Sasa tukisema kwamba, wakija wakate leseni, watakuwa wanatakiwa kulipa mara mbili, kitu ambacho tunaona kwamba ni bughudha. Kama atatakiwa kuvua mwaka mzima, anaruhusiwa kwa kufuata utaratibu ambao anatakiwa sasa akate leseni. Ahsante sana.

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa mipaka inayotambulika ni ya *deep sea*; kuna mipaka gani kati ya Zanzibar na Bara ili tufahamu wavuvi wasivuke kwenda upande mwingine?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika hapa tunachoangalia sio mipaka; kama mtu anatoka Zanzibar kuja Bara, tunataka kwanza tuhakikishe kwamba ni raiya wetu. Asitoke tu mtu yeyote kule tunakuja tunamkubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kama nilivyosema, tumejiwekea kwamba, kama mtu anatoka Zanzibar atakuwa anavua kule kwa kutumia leseni ya Zanzibar na huku Bara haitumiki. Kwa hiyo ni muhimu kabisa kwamba, atakapokuja tuweze kuiona hiyo leseni na tumhakiki. Kwa sababu tusipofanya hivyo, mali zetu za asili, tutastukia wageni ndio wanazifaidi na wengine tunaweza kupata watu wengine kuja kuvua huku kwetu, ambao wamefukuzwa kule Zanzibar na wanavua kwa njia za haramu. Sasa anapokuja tukamhakiki mwenzetu kutoka Zanzibar, inakuwa ni urahisi tunajua hawa ni ndugu zetu wamekuja kuvua basi. Kiasi tu cha kuhakiki kwamba ni mtu anatoka Zanzibar na sio wageni kutoka nje.

Na. 57

### **Makambi ya Wavuvi Kilombero**

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA (K.n.y. MHE. CASTOR R. LIGALLAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa miaka ya nyuma wavuvi Wilayani kilombero walizoea kwenda kuvua na kuishi kwa muda katika makambi na kurudi vijijini kwao baada ya kukamilisha kazi; na kwa kuwa hisi sasa makambi hayo yamegeuzwa kuwa nyumba za kudumu zinazowahusisha wanawake na watoto hali inayosababisha wavuvi kutorudi kwao hivyo kutelekeza familia zao zilizo vijijini ambazo hukosa mahitaji muhimu kama chakula na mavazi:-

(a) Je, serikali itasaidiaje Wilaya ya Kilombero katika kutatua tatizo hilo?

(b) Kwa kuwa samaki katika mito hiyo wamepungua sana kutokana na uvuvi haramu na kwamba maeneo hayo yako mbali na Maafisa Uvuvi; je, Serikali inaweza kuisaidia Wilaya kufanya *Fish Stock Assessment* kwa madhumuni ya kutoa ushauri wa rasilimali hiyo kwa kiwango endelevu?

(c) Je, Serikali ina habari kuwa baadhi ya *species* za samaki katika mito hiyo zinaendelea kutoweka kutokana na uvuvi mbaya unaofanyika katika mito hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Ligallama, Mbunge wa Kilombero, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa wavuvi wadogowadogo, ikiwa ni pamoja na wale wanaoishi kando kando ya Mto Kilombero wamekuwa na tabia ya kuhamahama kutoka eneo moja la uvuvi kwenda eneo lingine, kwa lengo la kufuata samaki kwenye maeneo wanayohisi kuwa na samaki wengi pamoja na soko. Aidha, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, baadhi ya wavuvi wamefanya makambi haya kuwa ya kudumu na wengine hata kutelekeza familia zao. Hivyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, pamoja na wadau wengine, itaendelea kuwaelimisha wavuvi hao juu ya athari za kutelekeza familia zao, pamoja na wajibu wao kwa familia kama wazazi na walezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003, Kanuni ya 12(11), inamtaka mvuvi kuvua kwenye eneo la Wilaya alikopewa leseni ama kwingine atakakoruhusiwa. Aidha, katika mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005 yanayofanywa na Wizara yangu, wavuvi hawataruhusiwa kupiga kambi ya uvuvi kwa muda unaozidi miezi mitatu kwenye eneo moja la uvuvi. Tunatarajia kuwa, Kanuni hiyo itakapoanza kutumika, itaondoa tatizo la wavuvi kupiga makambi ya kudumu katika maeneo ya uvuvi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, samaki wamepungua sana kwenye Mto Kilombero na mito mingine, pamoja na maeneo mengine ya uvuvi. Kwa kiasi kikubwa, chanzo cha tatizo hili ni uvuvi haramu wa kutumia nyavu zenye macho chini ya nchi tatu na kokoro. Aina nyingine za uvuvi haramu kama vile kupiga katuli (kutibua maji kwa lengo la kuwafukuza samaki waingie kwenye mtego wa uvuvi). Sawia na kusimamia uzingatiaji wa Sheria na Kanuni za Uvuvi, Serikali itaendelea na jitihada za kuelimisha jamii ya wavuvi, kuhusu madhara ya kutumia zana haramu za uvuvi ili kupunguza uharibifu wa rasilimali ya uvuvi unaotokana na matumizi ya zana hizo, hususan katika Wilaya ya Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mkakati wa kutathmini wingi wa samaki (*Fish Stock Assessment*) katika maeneo ya wavuvi nchini, kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, Wizara yangu itahamasisha Serikali za Vijiji, pamoja na jamii ya wavuvi wanaoishi kandokando mwa mialo ya bahari, maziwa na mito kuanzisha Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vijulikanavyo kama *Beach Management Units (BMUs)*, ambavyo vinatambulika kisheria.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua tatizo la kupungua na hata kutoweka kwa baadhi ya aina (*species*) mbalimbali za samaki katika maeneo mengi ya

uvuvi nchini. Kutokana na sababu nilizoieleza hapo mwanzoni, kinachotakiwa ni wananchi, hususan jamii ya wavuvi, kufanya uhifadhi thabiti wa rasilimali hiyo na mazingira yake. Kwa kufanya hivyo, samaki wanaoonyesha kupungua na hata kutoweka, watarejea katika hali ya kupatikana kwa wingi kama ilivyotokea kwa samaki aina ya Furu na Ningu katika Ziwa Victoria. Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, pamoja na Wananchi, itachukua hatua hizo za uhifadhi ili kurekebisha hali hiyo.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa samaki wengi katika mito hiyo ni wa jamii inayojulikana katika lugha ya *zoology (chichilide)*, wenye tabia ya kutengeneza viota vya kutagia mayai; na kwa kuwa zana za uvuvi kama makokoro hugaribu viota hivyo na kuharibu kabisa mazalia ya samaki; je, Serikali itakuwa tayari kuleta Muswada hapa Bungeni wa Sheria kupiga marufuku matumizi ya makokoro katika mito?

Swali la pili, kwa kuwa wavuvi wengi wana familia zao vijijini; na kitendo cha wao kukaa kwa muda mrefu bila kurudi vijijini kunazifanya familia hizo kulelewa na akina mama tu kwa muda mrefu sana; je, Serikali ina mwongozo gani kuhusu suala hili mtambuka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Uvuvi Tanzania, inakataza kabisa kutumia makokoro katika kuvua na hivyo, kuharibu viota na sehemu nyingine za kutagia samaki. Kwa hiyo, kinachotakiwa hapo siyo kutunga Sheria; Sheria ipo pale pale.

Kwanza, ni kuhamasisha wananchi waelewe kwamba, kuvua kwa kutumia makokoro kunaharibu kabisa mazingira ambayo samaki wanatagia, lakini pale ambapo inabidi, Sheria itumike ili wale wanaofanya hivyo, wachukuliwe hatua za kisheria na mpaka sasa hivi mtu akipatikana anavua kwa kutumia makokoro anachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu familia kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba, sasa hivi tunazifanyia marekebisho kanuni zetu za uvuvi; itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kwenda kupiga kambi. Baada ya miezi mitatu, tutafanya utaratibu wa kukagua kama mtu atapatikana pale inabidi aondoke. Kwa hiyo, kwanza tutahamasisha na pale itakapoonekana inashindikana, Sheria itachukua mkondo wake.

## Hali ya Daraja la Mkapa

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa Daraja la Mkapa ni kiungo muhimu sana kwa Mikoa ya Kusini (Lindi na Mtwara) na kadhalika; na kwa kuwa iligundulika mapema kuwa nguzo moja ya daraja hilo ina ufa:-

(a) Je, pamoja na dosari nyingine katika daraja hilo zimerekebisha, kama bado ni kwa sababu gani?

(b) Je, Makandarasi waliojenga daraja hilo wanahusika vipi na dosari hiyo?

(c) Kwa kuwa barabara kati ya Daraja la Mkapa na Somanga siyo nzuri na majambazi hutumia mwanya huo kupora abiria; je, ni hatua gani imefikiwa ya kumpata Mkandarasi wa kujenga kipande hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Jimbo la Liwale, ninapenda kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Rufiji ulihusisha ujenzi wa daraja kuu moja, lenye urefu kwa meta 970.5, ambalo kwa sasa linajulikana kama Daraja la Mkapa; ujenzi wa madaraja madogo manne na ujenzi wa barabara kilometa 14 kwa kiwango cha lami. Mkataba wa ujenzi wa mradi huu, ulisainiwa mwezi Desemba, 1997 na muda wa Mkataba ulikuwa miezi 24. Hata hivyo, Mradi huo ulikamilika mwezi Septemba, 2003.

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mradi huu, dosari ya kitaalam ilijitokeza kwenye daraja mojawapo kati ya madaraja manne yale madogo. Daraja hilo lina urefu wa meta 90 na liko umbali wa meta 295, Kusini mwa Daraja Kuu la Mkapa. Dosari iliyojitokeza kwenye daraja hilo ni raba (*rubber bearings*) zilizopo juu ya nguzo ya mwisho, upande wa Kaskazini mwa daraja inayopokea sehemu ya juu ya daraja (*deck*), kuwekwa vibaya. Dosari hii ilisababisha nguzo hiyo kuyumba kuelekea Kusini baada ya kukamilisha ujenzi wa tuta la udongo. Dosari hiyo pia ilisababisha sehemu ya juu ya nguzo hiyo kugusana na *deck* na kusababisha nyufa kwenye nguzo. Ili kuzuia sehemu hizi mbili zisigusane, Mkandarasi aliweka vipande vya mbao kutenganisha sehemu hizi ambazo kawaida zinapaswa kutenganishwa na uwazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mhandisi Msimamizi anadai kuwa tatizo hilo inawezekana linasababishwa na udongo chini ya daraja, kutokuwa imara kuhimili tatizo uzito wa tuta, lakini ameshindwa kuthibitisha madai hayo.

Mkandarasi anadai kuwa, yeye alijenga kulingana na michoro ya mkataba kinyume na ukweli kuwa raba juu ya nguzo ziliwekwa sehemu tofauti na mchoro unavyotaka na hatua hiyo ndiyo iliyosababisha nguzo kushindwa kuhimili msukumo wa udongo wa tuta la barabara.

Wizara ilimwagiza Mkandarasi na Mhandisi Msimamizi kuziba nyufa zilizojitokeza na kuondoa vipande vya mbao vilivyowekwa kati ya 'Deck' na nguzo husika kuzuia kugusana kwa sehemu hizi mbili za daraja kabla halijapokelewa.

Kazi ya kuziba nyufa ilikamilishwa, hata hivyo, Mkandarasi, pamoja na Mhandisi Mshauri, hawakuchukua hatua ya kuondoa vipande vya mbao kama walivyoagizwa. Wizara imechukua hatua ya kutopokea daraja hilo dogo na hivyo kutowalipa hati zao za madai ya mwisho mpaka upatikane ufumbuzi wa kudumu wa kasoro hizo.

Ili kupata ukweli wa tatizo hili, Wizara imeingia Mkataba na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kupitia Taasisi yake ya *BICO*, kufanya uchunguzi na kisha kuishauri Serikali kama daraja husika linakubalika. Taarifa ya Wataalam wa *BICO* ndiyo itakayoainisha waliosababisha dosari hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, pamoja na marekebisho yake kama ifuatavyo:-

(a) Hadi sasa hakuna dosari nyingine ambayo imekwisha jitokeza katika Daraja Kuu la Mkapa na wala kwenye madaraja hayo mengine madogo.

(b) Uchunguzi wa Kitaalam unaofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Taasisi yake ya *BICO* ukikamilika, ndiyo utakaodhihirisha ni kwa kiasi gani Mkandarasi na Mhandisi Mshauri walihusika na dosari hizo.

(c) Matayarisho ya ujenzi wa barabara kati ya Daraja la Mkapa (Ndundu) hadi Somanga yameanza. Kwa sasa tumekamilisha majadiliano na Mkandarasi aliyependekezwa kujenga sehemu hiyo na tunasubiri ridhaa ya Mfadhili wa Mradi huu (*Kuwait Fund*), ili mkataba wa ujenzi uweze kusainiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, anajibu kwa uzoefu kwa Wizara ile aliyotoka. Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, swali la nyongeza na baadaye nitamwita Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri.

La kwanza, je, tatizo kama hilo lililojitokeza katika Daraja hilo la Mkapa, Serikali inachukua hatua gani ili lisiweze kutokea tena hasa kwa Makandarasi hao tunaoendelea kuwapa kazi na baadhi yao wameshaonyesha udhaifu?

La pili, kwa kuwa Daraja la Mkapa ni kiungo kizuri sana kwa barabara itokayo Nangurukuru kwenda Liwale; na kwa kuwa ni dhamira ya Serikali barabara hiyo ya

kwenda Nangurukuru kwenda Liwale ipitike kipindi chote cha mwaka na mwaka huu imejifunga; je, Serikali ina mpango gani kuwaridhisha Wananchi wa Liwale ili waweze kuitumia barabara hiyo kwa kipindi chote cha mwaka kama ilivyoahidiwa katika dhamira zake? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninapenda tu nimfahamisha Mheshimiwa Hassan Kigwalilo kwamba, nia ya Serikali kuweka *consultant* kuangalia ujenzi wa barabara ni kuhakikishia kwamba, masuala hayo hayajitokezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii niwaombe *consultants* wanaosimamia ujenzi wa barabara, wahakikishe wanasimamia kikamilifu na Serikali itachukua hatua zifaazo kuhakikisha kwamba, suala hili linapewa uzito unaofaa na halitatokea tena katika madaraja mengine ambayo yatajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ninapenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara kwa kupitia *TANROADS*, itahakikisha kipande hicho cha barabara ambacho kipo katika hali ambayo siyo nzuri kinapitia wakati wote. Kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, tunachosubiri hapa ni kupata *no objection* na kutia saina *contract* ili ujenzi uanze mara moja.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninapenda kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya Nangurukuru kwenda Liwale asilimia kubwa ipo katika Jimbo la Kilwa Kaskazini pale kwenye Mlima Tembo na ni mlima kubwa sana ambapo ajali nyingi huwa zinatokea pale na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga mara ya mwisho alisema kwamba angeweza kuweka lami; je, mpango huo upo karibu kukamilika ili wananchi wa sehemu zile waweze kunusuru mali zao na wenyewe kujinusuru? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda ni Serikali siyo Naibu Waziri, anayeweza kuweka lami.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda kwamba, nia na ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu ipo pale pale; fedha zikipatikana masuala ya kuweka lami barabara, si hiyo tu na barabara nyingine zote ambazo zinakidhi mahitaji ya wananchi kupeleka mazao yao na shughuli zao zitashughulikiwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimepewa *ki-note*, ninakubaliana na Mbunge aliyesema kwamba, tukiwa humu ndani, Wabunge ambao hawazungumzi wasilete kelele kwa kuzungumza au kujadiliana wao wenyewe. Nitawatajia baadaye Kanuni inayohusika.

## **Ujenzi wa Barabara ya Dodoma – Mtera – Iringa**

**MHE. YONO S. KEVELA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Dodoma kwenda Iringa kupitia Mtera ni muhimu sana kiuchumi:-

- (a) Je, ni lini barabara hiyo itajengwa?
- (b) Je, upembuzi yakinifu unaonyesha ni kiasi gani cha fedha kinahitajika kwa kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Jimbo la Njombe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa kazi ya upembuzi yakinifu, pamoja na usanifu wa kina, ulitiwa saini kati ya Serikali na Mhandisi Mshauri tarehe 22 Agosti, 2007. Mhandisi Mshauri alianza kazi hiyo tarehe 22 Septemba, 2007. Kazi hiyo inatarajiwa kufanyika kwa muda kwa miezi 18 hivyo, itakamilika tarehe 22 Machi, 2009. Sambamba na kuendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu, Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa lengo la kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami, mara kazi ya usanifu itakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mhandisi Mshauri bado anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu, pamoja na usanifu wa kina, kiasi halisi cha fedha kinachohitajika kwa ujenzi wa barabara, kitajulikana mara baada ya kukamilisha usanifu wa kina.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hili suala la upembuzi yakinifu kwa muda mrefu toka enzi za Awamu ya Kwanza wanasema upembuzi yakinifu; huu upembuzi yakinifu inawezekana sasa tunawadanganya wananchi; je, utaisha lini?

Swali la pili, kwa vile matatizo ya uchambuzi yanafanyika katika ile Barabara ya Njombe kwenda Makete; na mpaka sasa hivi ni kilio kikubwa; haipitiki kabisa na Ubunge wangu umekuwa mashakani kwamba siwasemei kuhusu barabara hii; je, Serikali inasema nini kuhusu hii Barabara ya Njombe - Makete kupitia pale Igosi na Igagala kwa sababu iko chini ya *TANROAD*; ni lini itarekebishwa kwa sababu hali sio nzuri; Ubunge wangu unatiliwa mashaka?

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, unamsema na Naibu Spika.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niwaombe wananchi wasimpe tabu; matatizo tuliyonayo ni uhaba wa fedha ambayo ote tunaelewa. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, *consultant* anamalizia *detail design* na *bidding documents* kwa sababu ni kazi mbili kwa pamoja na anayefanya ni *COI Consultant*, lakini Serikali imewa-*approach EDB* na *World Bank* na wameonyesha nia ya kufadhili Mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *detail design* ilipaswa kumalizika mwezi uliopita, lakini haijamalizika; ninafikiri itamalizika muda wowote na ikimalizika, hiyo ndiyo itakayotupa *cost* ya barabara hii ili *EDB* na *World Bank* wawe *approached* kufadhili Mradi huu. Ninaomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira; Serikali inashughulikia masuala yake.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kuhusu Barabara ya Iringa kuja Dodoma.

Je, Waziri anaweza kuwathibitishia Wananchi wa Mkoa wa Iringa kwamba fedha za kutosha zitawekwa katika makisio ya mwaka 2008/2009 ili kazi iendelee na kuondoa danadana au tuseme porojo ambazo zilikuwa zikiendelea kwa muda wa miaka kumi iliyopita kuhusu barabara hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri na mbaya zaidi wanaweka kifusi cha kulimia chai!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaomba nitoe wito kwa Mameneja wa *TANROADS* wahakikishe wanapoweka kifusi katika barabara, wasimamie *consultants* au *contractors* wasiweke kifusi cha tope ambacho hakikidhi mahitaji.

Pili, ninapenda nimhakikishe Mheshimiwa Galinoma kwamba, kama tulivyokubaliana katika masuala yetu ya barabara kwamba, huu ni wakati muafaka sasa tutenge fedha katika bajeti yetu ili tutengeneze barabara zetu badala ya kusubiri wafadhili. Barabara nyingi zimejengwa kwa mtindo huu, lakini kwa sababu fedha zinazotakikana kujenga barabara ni nyingi sana, ndio maana tunawa-*approach* wafadhili mbalimbali, ku-*supplement efforts* za Serikali.

Vilevile nitamshauri sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, ahakikishe kwamba, barabara alizozitaja Mheshimiwa Galinoma, pamoja na barabara ya Mheshimiwa Kigwalilo, zinapewa uzito unaofaa kwa mwaka huu.

Na. 60

### **Uchaguzi wa Majaji Katika Mahakama ya Rufaa**

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1979 Tanzania ilianzisha Mahakama ya Rufaa kufuatia kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na kwa kuwa Mahakama imefanywa kuwa ya Muungano ijapokuwa hapo awali suala la Mahakama halikuwa katika orodha ya Mambo ya Muungano.

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika kuwachagua majaji katika Mahakama hiyo?

(b) Je, kwa hivi sasa Mahakama hiyo ina majaji wangapi kutoka Tanzania Zanzibar?

(c) Je, Baraza la Wawakilishi Zanzibar linaweza kuwa na Mamlaka ya Kisheria ya kudhibiti upeo wa Mahakama hiyo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a), (b) na (c), ninaomba nitoe maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliundwa mwaka 1979, kwa mujibu wa Mabadiliko ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 117(1). Mabadiliko hayo yalifanyika kwa kufuata masharti yote yaliyowekwa na Katiba, kwa ajili ya kufanya mabadiliko katika orodha ya kwanza inayohusu mambo ya Muungano.

Baada ya maelezo hayo ya ujumla, sasa ninapenda kulijibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuwateua Majaji wa Rufani, umeanishwa katika Ibara ya 118(2) na (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa mujibu wa utaratibu huo, Majaji wa Rufani huteuliwa na Rais baada ya kushauriana na Jaji Mkuu. Jaji Mkuu ameelekezwa na Ibara ya 116(2) ya Katiba, kushauriana na Jaji Mkuu wa Zanzibar katika uendeshaji wa shughuli za Mahakama ya Rufani kwa ujumla na hususan kuhusu uteuzi wa Majaji wa Rufani.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya Majaji wa Rufani kutoka Zanzibar kwa sasa ni wawili kati ya 12 na mmoja wao ndiye Jaji Mkuu wa Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 107 inatamka wazi kwamba, Mahakama zote, ikiwa ni pamoja na Mahakama ya Rufani, katika utendaji wake, hufuata Katiba zote mbili; yaani ile ya Jamhuri ya Muungano na ile ya Zanzibar, pamoja na Sheria na Kanuni zote za Jamhuri ya Muungano. Hivyo, kazi ya Mahakama ya Rufani ni

kusikiliza na kutoa uamuzi juu ya kila rufaa inayoletwa mbele yake, kutokana na hukumu ya Mahakama Kuu au Mahakama yoyote ya chini, iliyopewa mamlaka maalum ya Mahakama Kuu. Maamuzi hayo yatazingatia Katiba na Sheria kama zilivyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na ile ya Zanzibara ya Mwaka 1984, udhibiti wa upeo wa Mahakama hii upo katika utungaji wa sheria. Kwa maana hiyo, Baraza la Wawakilishi kupitia Sheria linazotunga, lina mamlaka kisheria kudhibiti upeo wa Mahakama ya Rufani.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mwanasheria Mkuu, ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna pande mbili za Muungano na Mwanasheria ametueleza Majaji wa upande mmoja ni kumi na upande mwingine ni wawili; je, swala hili limezingatia Muungano?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoelezea katika jibu langu la msingi ni kwamba, Jaji Mkuu wa Mahakama ya Zanzibar huwa anashirikishwa katika uteuzi wa Majaji ya Mahakama ya Rufani. Kwa hiyo, masuala ya Muungano huwa yanazingatiwa wakati wa uteuzi wa Majaji ya Mahakama ya Rufani.

Na. 61

### **Mahakama kama Mhimili wa Dola**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuza:-

Kwa kuwa Mahakama ni Mhimili wa Tatu wa Dola; na kwa kuwa Mhimili wa Pili wa Dola ni Bunge ambalo tayari lina mfuko wake:-

Je, lini Serikali itaipaitia Mahakama mfuko wake ili nao waweze kujipangia mambo yao?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa, Mahakama ya Tanzania ni Mhimili wa Tatu wa Dola na ni kweli pia Bunge la Tanzania ambalo ni Mhimili wa Pili wa Dola lina mfuko wake. Aidha, Mahakama ya Tanzania kama Mhimili wa Dola, ingependa sana kuwa na mfuko wake kama ilivyo kwa Bunge. Serikali inaupokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tutaufanyia kazi ili Mhimili huo nao uwe na mfuko wake pindi hali itakaporuhusu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naib Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Vifaa vya kazi vya Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa vipo katika hali duni sana; Serikali haioni kwamba, kuna umuhimu tena wa haraka, kuweka utaratibu wa *Hansard* kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za kesi ili kuwaondoa Majaji katika kazi ya kuandika kwa mkono ambayo wanaifanya hivi sasa?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wenzetu wa Mahakama wana matatizo; kama alivyonieleza Mheshimiwa Mbunge, tatizo hili sasa hivi linafanyiwa kazi, Mahakama ipo chini ya Mpango wa *Legal Sector Reform Program*, ambapo mojawapo ya kazi zake ni kuhakikisha kwamba, inapata mazingira mazuri ya watendaji wa kazi. Kwa hiyo, jambo hilo ambalo amezungumza Mheshimiwa Mbunge linafanyiwa kazi.

Na. 62

### **Maji ya Bwawa la Mtera**

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika msimu wa mwaka 2006/2007 kumekuwepo na mvua za kutosha zilizosababisha Bwala la Mtera kujaa maji mpaka kulazimika kuyamwaga; na kwa kuwa maji hayo kitaalam yanaweza kutumiwa kuzalisha umeme katikati kabla ya kufika Kidatu ambapo yanatumika pia; na kwa kuwa wakati huu wa neema maji yanapotea bure baharini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka bwawa dogo (*mini-dam*) na mashine ambazo kwa mchana zinazalisha umeme na usiku kugeuka mota ili kurejesha maji kwenye bwawa kubwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, ninaomba nitoe maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kina cha juu ambacho kinaweza kufikiwa na maji katika Bwawa la Mtera bila kusababisha uharibifu ni mita 698.5, juu ya usawa wa bahari. Kina hiki huweza kufikiwa iwapo kunakuwepo mvua nyingi katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na Mikoa ya Kati ya nchi. Iwapo kiwango hiki kikifikiwa, *TANESCO* hulazimika kufungulia mageti ya kuzuia maji, kwa lengo ya kupunguza maji ili yasiweze kuleta madhara ya kubomolewa kwa kingo za bwawa na hatimaye kusababisha hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vinavyozalisha umeme mchana na usiku kugeuka kuwa pampu za kurejesha maji kwenye bwawa kubwa, vinajulikana kitaalam

kama *pump storage hydro plants*. Kwa takriban miaka 50 iliyopita, teknolojia hiyo imekuwa ikitumika sehemu mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zilizoendelea zimejenga vituo vya *pump storage hydro plants* kwa lengo la kutunza maji (*water optimization*) na pia ili kurekebisha voti za umeme katika mifumo mikubwa ya umeme (*voltage fluctuation controls*), wakati wa matumizi makubwa ya umeme wakati wa mchana. Mfano wa vituo hivyo ni Tianhuangping nchini China, Dinowring nchini North Wales na Arce nchini Slovenia.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama ya ujenzi wa *pump storage hydro plants* ni takriban mara mbili ya ujenzi wa kituo chenye uwezo sawa wa kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu ya maji. Aidha, kituo cha *pump storage hydro plants* hutumia umeme ufikao asilimia 75 ya uwezo wa uzalishaji wake, kinapotumika kama pampu ya kusukuma maji wakati wa usiku. Kutokana na sababu hii, inahitajika mifumo mikubwa ya umeme wa gridi (*huge grid networks*), yenye umeme wa ziada wakati wa usiku ili kuendesha kituo cha *pump storage hydro plants* kwa lengo la kurudisha maji kwenye bwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za ujenzi wa kituo cha *pump storage hydro plants*, kati ya Mtera na Kidatu chenye uwezo wa kuzalisha Megawati 80 kama zinazozalishwa kwenye kituo cha Kidatu, utahitaji kiasi cha Dola za Marekani milioni 280. Aidha, kituo hicho kitahitaji kupewa Megawati 60 wakati za usiku, kitakapokuwa kinatumika kama pampu ya kurudisha maji katika Bwawa la Mtera. Kiasi hicho cha Dola za Marekani milioni 280, kinatosha kabisa kujenga kituo cha kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu za maji za Kituo cha Mpanga kilichopo Wilayani Njombe, ambacho kitaweza kuingiza Megawati zipatazo 140 kwenye gridi mpaka 160 na ambacho hakitahitaji umeme wa ziada wakati wa usiku kama ilivyo kwa kituo cha *pump storage hydro plants*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijawa na mpango wa kujenga *mini-dam* kwa ajili ya kujenga *pump storage hydro plants* kati ya Mtera na Kidatu kwa ajili ya kuzungusha maji, kutokana na ukubwa wa gharama za ujenzi wake na uendeshaji wa mitambo. Aidha, Gridi ya Taifa tuliyonayo, haina umeme wa ziada wakati wa usiku kutosheleza kuendesha *pump storage hydro plants*.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza, ikiwa Serikali haina mpango wa kujenga *mini-dam*; je, hili Bwawa la Mtera lililopo hivi sasa sina hakika mara ngapi katika kipindi cha miaka mitano linasafishwa kama *routine maintenance*; kutolewa matope na michanga inayojaa kwa ajili ya mvua ili hicho kina cha maji cha mita 698.5 kifikiwe?

Pili, ikiwa hilo bwawa halijasafishwa katika kipindi cha miaka mitano au kumi; je, hicho kina cha maji cha mita 698.5 haionekani kwamba kitakuwa ni cha uongo na ni *falls reading*, ambacho kinaweza kutusababishia kuona kwamba bwawa limejaa maji lakini hali halisi ni kwamba maji tunayosema kina chake hayatimii?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Habibu Juma Mnyaa, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sina idadi ya mara ngapi katika miaka mitano iliyopita bwawa hili limesafishwa, isipokuwa ninafahamu kwamba ni utaratibu wa *maintenance*, yaani matunzo ya bwawa hilo ambao unafanywa na *TANESCO*, isipokuwa sina uwezo sasa wa kukupa idadi kamili yaani mara ngapi katika miaka mitano iliyopita bwawa hilo limesafishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba anipe muda ili nifuatilie na watu wa *TANESCO* halafu nitamjibu swali hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la nyongeza la pili ni kwamba, inaawezekana kwa sababu ya kujaa matope labda tukawa tunapata *falls readings*; ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mnyaa kwamba, kwa kila siku yaani kila alfajiri, Wataalam wa *TANESCO* wanachukua vipimo vya maji yalivyo katika mto na wanaleta Makao Makuu ya *TANESCO* na Makao Makuu ya Wizara. Sasa ninaamini kabisa kwamba, vipimo wanavyotumia kwa mfano, leo wametupa vipimo ninadhani ni 697.5 sina hakika, lakini wao wameridhika navyo. Sasa ninaamini kabisa kwamba ni vipimo ambavyo ndivyo tunavyoendelea kutumia kulingana na kazi ya *maintenance* inavyofanywa kwa taratibu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama wao wanaridhika navyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge naye aridhike kwamba, wataalam wa *TANESCO* wanaridhika navyo hivi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea na swali linalofuata na kufuatana na muda atakachofanya Mheshimiwa Waziri ni kuleta maelezo ni mara ngapi waliweza kusafisha bwawa. Mheshimiwa Michael Laizer Lekule swali linalofuata.

Na. 63

### **Mrabaha Kutokana na Mgodhi wa Ruby Mundarara**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa Sekta ya Madini ni muhimu sana katika kukuza uchumi wetu; na kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imejitahidi kukusanya kodi ya madini ili kuendelea kuongeza Pato la Taifa na hatimaye kukua kwa uchumi wetu:-

(a) Serikali inapata *royalty* kiasi gani kutokana na Mgodu wa Ruby wa Mundarara kwa kipindi cha mwaka 2000 hadi 2005?

(b) Je, Serikali ina uhakika gani na madini ya Ruby yanayopatikana kwenye Mgodu huo?

(c) Kwa kuwa, Serikali imeagiza Mgodu kutoa *royalty* kwa vijiji vilivyoko kwenye eneo la Mgodu; je, Mgodu huo ambao hautoi chochote hauhusiki kwenye utaratibu huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, swali lake kama ifuatavyo:-

Kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, ninaomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgodu wa Mundarara ulioko Wilayani Longido, unamilikiwa na Kampuni ya Mundarara *Ruby Company Ltd.*, kwa kutumia leseni zake mbili zenye namba *GML 130/2002* na *GML 131/2002*. Mgodu huu huzalisha mawe ya *zoisite* na kiasi kidogo cha Madini ya *Ruby*. Kati ya mwaka 2002 hadi 2004, Kampuni ya *Paradiso Minerals* ilikuwa na mkataba wa uendeshaji wa Mgodu wa Mundarara. Aidha, Kampuni ya *Vith Arthvitawas* iliingia mkataba wa uendeshaji wa Mgodu huo tokea mwezi Oktoba, 2005 hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendeshaji wa Mgodu wa Mundarara kwa kipindi cha nyuma, umekuwa hauridhishi kutokana na matatizo ya uongozi na ukosefu wa mtaji wa kutosha na kuendesha Mgodu. Mabadiliko ya mara kwa mara ya Uongozi wa Mgodu yaliathiri uzalishaji katika Mgodu huo. Kuanzia mwaka 2001 hadi 2002, Mgodu ulifungwa na pia kuanzia mwezi Aprili, 2007 hadi sasa, hakuna uzalishaji unaofanyika katika Mgodu huo.

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapata mrabaha kutokana na uzalishaji unaotokana na mgodu na siyo kuwepo kwa mgodu wenyewe katika eneo hilo. Sheria ya Madini kwa Madini ya Vito (*Ruby*) yasiyosanifiwa (*rough gemstones*), imetoa sharti la asilimia tano kama mrabaha na kwa Madini mengine (*zoisite*) mrabaha si asilimia tatu. Kwa maana hii kati ya mwaka 2000 hadi 2005 kiasi cha *Ruby* na *Zoisite* zenye thamani ya US\$ 268,084.68 ziliuzwa. Serikali ilipata shilingi 8,357,600 kutokana na mauzo ya madini hayo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taratibu za Madini ya *Ruby* yanayouzwa nje yanawasilishwa kwenye Ofisi ya Madini husika, kwa ajili ya kuhakikiwa na kutathminiwa katika hatua hii hivyo, uhakika wa kasi na thamani uafahamika. Hii inatokana na Kampuni ya *Mundarara Ruby Company Ltd.* kuwasilisha taarifa za utendaji kazi zake Wizarani. Aidha, kabla ya kusafirisha Madini yaliyopatikana kutoka katika Mgodini wa Mundarara kama ilivyo kwa migodi mingine, kwenda nje ya nchi; madi hayo yalikuwa yakikaguliwa na kutathminiwa na Maofisa Madini, wakishirikiana na Maafisa wa *TRA* kabla ya kuyafunga kwa lakiri na kuyapatia kibali cha kuyasafirisha nje ya nchi (*export permit*).

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijatoa maagizo ya kutoa mrabaha kwa vijiji vilivyoko kwenye maeneo yanayozunguka mgodi kwa uongozi wa mgodi wowote hapa nchini, ukiwemo Mgodini wa Mundarara, kwa vile hakuna Sheria inayoelekeza kufanya hivyo. Mrabaha unatolewa kwa Serikali Kuu tu. Migodi yenye leseni kubwa za uchimbaji madini kama *Geita Gold Mine* ulioko Geita; *Bulyanhulu Gold Mine* ulioko Kahama; *North Mara Gold Mine* ulioko Tarime; *Golden Price* ulioko Nzega; na *Tulawaka Gold Mine* ulioko Biharamulo, ndiyo yenye Mikataba na Serikali (*Mining Development Agreements – MDAs*) na ndiyo ambayo huwajibika kutoa Dola za Marekani 200,000 kila mwaka kwa Halmashauri za Wilaya ilipo Migodi hiyo, kwa mujibu wa Mikataba hiyo na Sheria Ndogo za Halmashauri husika.

Serikali imekuwa ikizishauri Kampuni za Madini kusaidia shughuli za maendeleo katika vijiji vinavyozunguka migodi kwa ajili ya kuendeleza uhusiano mzuri kati ya vijiji na migodi husika. Tuna taarifa kuwa, Mgodini wa Mundarara umekuwa ukishirikiana na Serikali ya Kijiji cha Mundarara katika Miradi ya Shule, Maji na Zahanati. Mgodini umetoa mabati 100 kwa kila Shule za Msingi za Kitarini, Engarenaibo na Kata ya Longido. Katika Kijiji cha Mundarara, Mgodini umejenga madarasa mawili, umesaidia matengenezo ya kisima na umetoa lori kusaidia ujenzi wa Zahanati. Kwenye Kijiji cha Engarenaibo, Mgodini ulitoa shilingi milioni moja kwa ajili ya matengenezo ya pampu ya maji na hutoa lita 50 za dizeli kila baada ya wiki mbili kwa ajili ya pampu hiyo. Kwa ushirikiano na Mheshimiwa Diwani, Mgodini umetoa ajira kwa vijana wa kijijini wapatao kumi. Pamoja na Sheria zilizopo sasa ambazo haziruhusu migodi kutoa mrabaha kwenye vijiji vinavyozunguka migodi hiyo, Serikali iko kwenye mchakato wa kuziangalia upya, Sheria zinazotawala shughuli za madini nchini, ambapo Tume ya Rais ya Kuangalia Mfumo wa Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta ya Madini, inategemewa kukamilisha kazi yake mwezi huu wa Aprili, 2008.

Matokeo ya kazi ya Tume ya Rais, yatajumuishwa katika juhudi za Serikali kuifanyia marekebisho Sekta ya Madini, ambapo masuala ya mrabaha na ulipwaji wa kodi nyingine yataangaliwa kwa lengo la kuwawezesha wananchi wanufaike vizuri zaidi na Sekta ya Madini.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza na ninajaribu kuzingatia ombi lako

kwamba, Naibu Waziri ni mgeni kwa hiyo, tusimuulize maswali magumu, lakini mgodi wenye una kasheshe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Waziri anieleweshe kwamba, kwanza huu Mgodi ulikuwa ni wa umma, ambao ulikuwa chini ya *STAMICO*; naomba anieleweshe kama umeuzwa au umebinafsishwa kwa kampuni ipi? Majibu aliyotoa si kweli kwani Mgodi huu unazalisha sana kwa sababu uko katika kijiji ninachotoka.

Jambo la pili, kwa kuwa migodi mingine ya dhahabu Halmashauri wanapata asilimia kama alivyosema; je, katika migodi mingine kama hii Serikali haiwezi kuwasaidia Halmashauri kama Halmashauri ya Longido wapate angalau asilimia hata kama haifiki dola 200,000 lakini na sisi tupate asilimia kutokana na mapato yanayopatikana pale?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Lekule Laizer, Mbunge aw Longido, maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgodi wa Longido kama nilivyoeleza awali, ulibinafsishwa kwa Kampuni ya *Paradiso Minerals* na wao baadaye wakaingia mkataba wa uendeshaji na kampuni ya Vith toka mwaka 2005. Sasa haya ndiyo maeleo ambayo tulipokea sisi Wizarani, lakini kama kuna jambo linatokea kinyume na taratibu hizo, basi wanakiuka utaratibu kwa kuwa hawatuletei taarifa hizo za utekelezaji wa kazi. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Lekule Laizer kwamba, kwa taarifa hiyo aliyotupatia, sisi Wizarani tutaifanyia kazi, tuweze kujua kwa nini hatupati taarifa za utekelezaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hili suala la vijiji vinavyozunguka migodi hii kutokufaidika moja kwa moja na kuwepo kwa mgodi huo katika maeneo hayo, Wizarani yetu imeona na ndiyo maana tumesema tunasubiri tupate matokeo ya utafiti na taarifa itakayotolewa na Tume ya Rais na sisi Wizarani tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Lekule Laizer kwamba, kama nilivyosema, tutayajumuisha katika juhudi za Serikali za kuifanyia marekebisha Sekta nzima ya Madini ili wananchi hasa wale wanaozunguka maeneo hayo, wanufaike zaidi sana na Sekta ya Madini.

**NAIBU SPIKA:** Muda hautoshi na sitendi kuacha maswali. Mheshimiwa Waziri tafadhali jibu kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninataka kuongezea kidogo kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, hasa kuhusu jinsi ambavyo Serikali inaweza kuwasaidia Wananchi wa Longido kufaidika na kile kinachopatikana hasa kwenye migodi iliyopo kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ni huu ufuatao kwa kuwasaidia tu ndugu zetu wa Longido: Kimsingi wanaotakiwa kuanzisha huu mchakato ni wao wenyewe Halmashauri, Baraza la Madiwani wakae watunge sheria ndogo kulingana na Sheria ya mwaka 1982, inayozipa madaraka Halmashauri zetu kwanza, kuweza kutunga sheria kwa ajili ya kuona ni vyanzo gani ambavyo vinaweza kutusaidia na ndivyo ilivyofanyika katika hizo Halmashauri nyingine ambapo migodi hiyo ipo. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Wizara yetu, tusaidiane ku-*arrange* utaratibu unaofanyika halafu tuone ni jinsi gani wanaweza kunufaika na hilo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa tunakwenda Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Martha Mosses Mlata, hayupo badala yake Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo atauliza swali.

Na. 64

### **Mfuko wa Pembejeo**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. MARTHA M. MLATA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mfuko wa Pembejeo ulianzishwa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kukopeshwa pembejeo na zana za kilimo:-

(a) Je, tangu 2000 – 2005 wakulima wangapi Mkoani Singida waliomba mkopo na wangapi kati yao walikopeshwa kwa kila Wilaya?

(b) Je, ni nini kinachelewesha upatikanaji wa mikopo hiyo kwani wakulima wengi wanalalamika kuwa maombi yao hayashughulikiwi mapema?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mosses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2000 – 2005, waombaji wa mikopo kutoka Mkoa wa Singida walikuwa ni 14. Kati ya maombi hayo, manne ni ya pembejeo za kilimo na mifugo, yenye thamani ya shilingi 191,000,000, katika maombi mawili kutoka Manispaa ya Singida, matatu Singida Vijijini, mawili kutoka Manyoni na moja kutoka Iramba. Maombi mengine sita ni ya matrekta mapya yenye thamani ya shilingi 210,000,000, maombi mawili kutoka Wilaya ya Iramba na manne kutoka Manispaa ya Singida. Mikopo iliyotolewa kwa Mkoa wa Singida katika kipindi cha 2000 – 2005 ni minane na ilikuwa na thamani ya shilingi 103,500,000.00. Kati ya mikopo hii, mitano ni ya pembejeo za kilimo na mifugo yenye thamani ya shilingi 71,500,000.00 kwa mgawanyo kama ifuatavyo: Mikopo miwili ilitolewa kwa Wilaya ya Singida Vijijini,

miwili mingine kwa Manispaa ya Singida na mmoja kwa Wilaya ya Iramba. Mikopo mitatu ya ununuzi wa matrekta mapya yenye thamani ya shilingi 83,500,000.00 ilitolewa, miwili kwa Manispaa ya Singida na mmoja kwa Wilaya ya Iramba.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Pembajeo umeweka taratibu za kumwezesha mkopaji kupata mkopo wake haraka iwezekanavyo kama ifuatavyo:-

(i) Waombaji wanatakiwa kujaza fomu za maombi baada ya kutolewa tangazo na Halmashauri za Wilaya la kuweka mikopo na pembajeo za kilimo na mifugo kupitia Mfuko wa Pembejeo.

(ii) Maafisa Kilimo/Mifugo wa Wilaya wathibitishe kuwepo kwa shughuli zinaoombewa mikopo katika Wilaya husika.

(iii) Fomu za maombi ya mikopo na vielelezo vinavyohitajika ziwasilishwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko, ambapo huchambuliwa na kuwasilishwa kwenye Kikao cha Bodi ya Wadhamini wa Mfuko ili yaidhinishwe.

(iv) Maamuzi ya Bodi hutumwa kwa waombaji na kwenye Halmashauri za Wilaya husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo mingi hucheleva kupatikana kutokana na waombaji wanaopendekezwa kwa ajili ya kupewa mikopo kucheleva kukamilisha masharti ya mikopo. Kwa mfano, waombaji hutakiwa kupata dhamana inayokubalika kabla ya kupewa mikopo yao. Aidha, ninapenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, waombaji wa mikopo ni wengi kuliko uwezo wa Mfuko wa Pembejeo hivyo, kuna wakati waombaji hutakiwa kusubiri. Kwa mfano, katika msimu wa 2007/2008, maombi yaliyopokelewa yalikuwa na thamani ya shilingi 8.0 bilioni, lakini uwezo wa Mfuko kutoa mikopo kwa msimu ni wastani wa shilingi 5.0 bilioni.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa wakopaji wa Singida wanaonekana ni wachache sana ukilinganisha na Mikoa mingine; na kwa kuwa sababu za msingi Mheshimiwa Naibu Waziri amesema ni ukosefu wa pesa; je, Serikali haioni kwamba kwa kuwa sasa hivi wakulima wameamka kuna sababu ya kuongeza pesa hizi ili sasa wapate mikopo hiyo kwa lengo la kuongeza kilimo?

La pili, kwa kuwa wakulima wa Mkoa wa Singida inaonekana wanacheleva kupeleka maombi ya mikopo yao; inawezekana sababu ikawa ni elimu ndogo kwa wakulima hao; je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kutoa elimu kwa wakulima hawa wa Mkoa wa Singida ili waweze kujaza fomu za mikopo na kuzifikisha kwa wakati muafaka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Diana M. Chilolo kama ifuatavyo:-

Sababu za kutopata mikopo kwa wakati kama nilivyosema mwanzoni ni bajeti ndogo, marejesho yasiyoridhisha, wakopaji wanachelewa kurudisha mikopo tukiwemo sisi Wabunge wenyewe tunachelewa kurudisha mikopo, tunachelewa kutekeleza masharti kwa maana ya kama mtu ameomba na hajapeleka *documents* zinazohitaji, kwa mfano, andiko ama kuwa na hati miliki ama kuwa na ankara kifani, usipokuwa na hivyo vitu huwezi kupata. Kwa ujumla ni kwamba, siyo kwamba ni wachache waliopata, Singida wameomba wengi lakini wamepata wale ambao wametimiza yale masharti yanayotakiwa.

Ni kweli kabisa kuna haja ya kuongeza fedha na fedha hizi zinaongezwa mwaka hadi mwaka; msimu uliopita fedha zilikuwa chini ya bilioni tatu, lakini sasa hivi ni bilioni 3.5, yaani mwaka huu unaopita. Ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna haja ya kuwapa elimu wakulima wetu ili waweze kukopa zaidi. Elimu hii inaweza kutolewa na Halmashauri na sisi wenyewe kama tunavyozungumza hapa, ninadhani tunawaelimisha wananchi kuchukua mikopo.

Na. 65

### **Uboreshaji wa Kilimo**

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotembelea Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika aliagiza Wizara kutayarisha mikakati na mipango itakayoweza kubadilisha kilimo kuwa cha kisasa, chenye tija na kinachowaletea wananchi maendeleo; na kwa kuwa pia aliagiza Wizara kuhakikisha kuwa wakati wote wananchi hawafi na njaa: Je, hadi sasa hiyo mikakati na mipango imefikia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Rais, alipotembelea Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, alitaka tufanye mapinduzi makubwa ya kilimo kwa sababu kilimo ni sekta inayotegemewa na 80% ya Watanzania. Mheshimiwa Rais, aliagiza Wizara itayarisha mikakati itakayoweza kubadilisha kilimo kuwa cha faida, chenye tija na kinachoweza kuwaletea wananchi maendeleo.

Mambo muhimu aliyosisitiza Mheshimiwa Rais na hatua za utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Moja, kuongeza matumizi ya zana za kilimo; katika kipindi cha kuanzia Januari, 2006 hadi Desemba, 2007 jumla ya matrekta makubwa 464 na matrekta madogo 325 yameingizwa nchini na Sekta binafsi. Katika mwaka 2007/2008, hadi Machi, 2008 jumla ya matrekta makubwa 80 yamekopeshwa kwa wakulima kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo.

Mbili, kuweka kipaumbele kwenye kilimo cha umwagiliaji maji; kati ya mwaka 2005/2006 na 2006/2007, eneo la hekta 23,953 liliendelezwa na hivyo kufanya eneo linalomwagiliwa kuwa hekta 273,945. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa eneo la hekta 125,579 unafanyika katika sehemu mbalimbali nchini.

Tatu, kuongeza matumizi ya mbegu bora; ili kuongeza upatikanaji na matumizi ya mbegu bora, mwaka 2006/2007, Serikali ilitenga shilingi bilioni 2.0 kwa ajili ya kutoa ruzuku ya mbegu bora na mwaka 2007/2008 shilingi bilioni 1.5 zimetengwa. Aidha, miche bora ya Kahawa na Chai iliingizwa kwenye utaratibu wa ruzuku, ambapo mwaka 2007/2008 shilingi bilioni 1.0 zilitengwa. Wakala wa mbegu umeanzishwa ili kuwa chombo cha kuzalisha, kusambaza na kuratibu usambazaji mbegu nchini.

Nne, kuongeza matumizi ya mbolea; ili kuongeza upatikanaji na matumizi ya mbolea, Serikali inatoa ruzuku. Bajeti ya ruzuku ya mbolea iliongezwa kutoka shilingi bilioni 7.486 mwaka 2005/2006 hadi kufikia shilingi 16.5 katika mwaka 2006/2007. Mwaka 2007/2008, shilingi bilioni 14.5 zimetengwa kwa ajili ya ruzuku ya mbolea. Hata hivyo, kiwango cha mbolea inayopewa ruzuku kimepungua kutokana na kupanda sana kwa bei ya mbolea kwenye Soko la Dunia. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na wawekezaji kuhusu uwezekanao wa kujenga kiwanda cha mbolea nchini. Hata hivyo, Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu, kinazalisha mbolea ya *phosphate* ya unga na hivi karibuni kimeanza kuzalisha mbolea ya *phosphate* ya chengachenga, ambayo itakuwa rahisi kwa mkulima kuitumia kuliko ya unga. Mbolea hii, bei yake ni nafuu sana ikilinganishwa na *DAP* inayoagizwa nchi za nje.

Tano, matumizi ya dawa za kudhibiti visumbufu vya mimea; Serikali ilianza kutoa ruzuku ya dawa mwaka 2006/2007, ambapo shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya dawa za korosho zilitolewa na mwaka 2007/2008, zilitolewa shilingi bilioni 2.6 kwa ajili ya dawa za pamba na korosho. Aidha, kila mwaka Wizara inagharamia dawa za kudhibiti milipuko kama panya, kwelea kwelea na viwavi jeshi.

Sita, kuwaandaa wakulima wenye ujuzi (*Skilled Farmers*); ili kufikisha utaalum kwa wakulima na kuwezesha kuandaliwa kwa wakulima wenye ujuzi (*Skilled Farmers*), Serikali imeongeza ajira kwa ajili ya wataalamu wa ugani na kuanza kuboresha mazingira ya kazi. Hadi Desemba, 2007 wataalamu wa ugani walioajiriwa walikuwa 308. Aidha, wakufunzi 89 wameajiriwa na wakufunzi 904 wameanza mafunzo vya uoni. Mashamba Darasa yaliendelea kuanzishwa na kuimarishwa. Hadi mwezi wa Desemba, 2007 jumla ya Mashamba Darasa 1,091 yenye jumla ya wakulima takriban 40,000 yameanzishwa

katika Mikoa yote nchini na yanatumika kuwafundisha wakulima kanuni za kilimo bora cha mazao.

Saba, kuwapatia wakulima masoko ya uhakika kwa mazao yao; Wizara inashughulikia suala la masoko ya mazao ya wakulima kwa kuimarisha Vyama vya Ushirika ili viweze kukusanya mazao ya wakulima. Katika mwaka 2007/2008, Wizara ilianza kwa kuviimarisha Vyama vya Ushirika katika maeneo yanayolima korosho ili kuviwezesha kufanya biashara ya ununuzi wa korosho kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani. Madhumuni ya zoezi hili ni kudhibiti dhuluma ya bei ambayo baadhi ya wanunuzi walikuwa wanawafanyia wakulima. Mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani, utendelezwa kwenye mazao mengine nchi nzima.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza, lakini pia ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais aliitembelea Wizara hii na kuagiza kwamba, ijtahidi kubadilisha kilimo cha nchi hii ili kiwe ni cha kisasa, chenye tija na kitakachoweza kuwaletea wananchi maendeleo. Ukweli ni kwamba, katika Pato la Taifa hivi sasa mchango wa kilimo unazidiwa na mchango wa utalii na mchango wa Madini na kwa takwimu za Benki Kuu mchango wa kilimo karibu ni sawa tu na mchango wa bandari zetu. Sasa je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubali kwamba ule msemu wa zamani kwamba “kilimo ni uti wa mgongo” sasa umepitwa na wakati?

La pili, Wizara inajua kabisa katika Wilaya ya Kongwa kuna Soko la Kimataifa pale Kibaigwa, lakini Serikali haijajenga ma-*godown* yoyote yale kwa ajili ya ku-*store* chakula kingi kupitia *SGR*; wala haiishawishi *World Food Program* au *AFO* kununua mazao pale; kwa nini Wizara haitumii fursa ya kuwepo kwa Soko la Kimataifa pale Kibaigwa vizuri kama inavyotakiwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Job Y. Ndugai kama ifuatavyo:-

Kilimo bado ni uti wa mgongo wa Taifa hili kwa sababu kama nilivyoeleza mwanzoni, asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo.

Nishati na utalii kuwa zimekuwa na asilimia kubwa ya kuchangia katika Pato la Taifa ni dalili nzuri ya nchi inayoendelea, nchi maskini inategemea kwa kiwango kikubwa sana uchumi wake kwenye kilimo, lakini nchi zinazoendelea zinakuwa na masuala mengine kama nishati, madini na viwanda vinachukua asilimia kubwa. Serikali itaendelea kuimarisha kilimo kusudi tuwezi kuuza nje kwa wingi, lakini vilevile kulinda *food security* kwa nchi. Kwa hiyo, suala la kutoka asilimia 46 kushuka mpaka asilimia 26 ya mchango wa kilimo si la kutisha ni jinsi tunavyoendelea.

La pili, suala la kujenga maghala linatakiwa lianze kwenye Halmashauri husika, waweke vipaumbele kwa kutumia fedha za *DADPS* na *ASDP*, wanaweza kujenga maghala na Serikali inaweza kuwasaidia kwa kutumia wadau mbalimbali. Serikali itaendelea kuwashawishi *World Food Program* waweze kununua chakula maeneo hayo.

Na. 66

### **Utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa asilimia sabini ya bajeti ya kawaida na asilimia mia moja ya bajeti ya maendeleo inafanya manunuzi ya vifaa na huduma za kandarasi za ujenzi:-

- (a) Je, Sheria ya Ununuzi wa Vifaa vya Umma inaeleweka kwa wadau wote?
- (b) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Halmashauri nyingi zinazoshindwa kufuata taratibu hizo kutokana na kukosa elimu na ubinafsi wa *PPRA*?
- (c) Je, Bodi ya *Public Procurement Regulatory Authority* inawezeshwa vya kutosha kufuatilia shughuli zake?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, sehemu kubwa ya fedha za bajeti ya kawaida na ile ya maendeleo, zinatumiwa katika kufanya manunuzi ya vifaa, huduma na kandarasi za ujenzi. Kwa maana hiyo, kuna haja kubwa kwa wadau kuielewa kwa umakini Sheria ya Ununuzi ya Umma ya mwaka 2004.

Kutokana na umuhimu huo, Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma imeanza kutoa elimu kwa wadau mbalimbali, juu ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ili iweze kueleweka. Wadau walioelimishwa ni pamoja na Wafanyakazi na Watendaji wa Serikali Kuu, pamoja na baadhi ya wakandarasi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, imeandaa utaratibu wa kuwaelimisha Wadau na Watendaji wa Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi ya Umma.

Mamlaka na TAMISEMI, zinafanya uchambuzi wa kina ili kuelewa matatizo ya msingi yaliyomo ndani ya Halmashauri, kwa lengo la kuandaa mkakati wa kukabiliana nayo na hatimaye kuziwezesha Halmashauri kuweza kufanya manunuzi bila ya matatizo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaiwezesha vya kutosha Mamlaka ya Ununuzi ya Umma ili iweze kutekeleza majukumu yake. Tokea kuanzishwa kwa Mamlaka, Serikali imeipatia Mamlaka fedha ambazo zimeiwezesha kukamilisha ajira, kununua vitendea kazi muhimu na kuandaa mikakati na mifumo mbalimbali katika Sekta ya Ununuzi wa Umma.

Mwaka 2006/2007, Mamlaka ilipatiwa shilingi 3.5 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 1.686 bilioni kwa ajili ya maendeleo (ADB) na mwaka 2007/2008, shilingi 3.5 bilioni za kawaida na shilingi 2.48 bilioni kwa ajili ya maendeleo.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wamewapatia mafunzo watendaji katika kuijua Sheria ya Manunuzi; je, ni watendaji wangapi waliopata mafunzo na kutoka taasisi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, sheria hii ambayo mtu akienda kinyume inamtoza Sh. 500,000/= ambacho kwa hali ilivyo hivi sasa ni kima kidogo; je, kuna mpango gani wa kuibadilisha sheria hii ili iende na wakati tulio nao hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, toka mwaka 2005 hadi sasa jumla ya watendaji 670 wamepatiwa mafunzo juu ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni kweli kuwa sheria hii inatoa adhabu ya Sh. 500,000/=, lakini vilevile imeeleza kwamba kuna kifungo cha miaka mitatu au vyote, kwa hiyo, inategemea na uzito wa suala lenyewe. Hakimu anaweza kutoa fidia Sh. 500,000/= au kifungo cha miaka mitatu au vyote. Lakini nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna haja ya kupitia upya (*review*) hiki kiwango ili kiwe kikubwa zaidi.

Na. 67

### **Mahitaji ya kuanzishwa kwa Benki ya Maendeleo Nchini**

**MHE. ELISA D. MOLLEL** aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo ni sekta kiongozi katika uchumi wa Taifa letu; na kwa kuwa kilimo kinatoa ajira kwa zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania:-

Je, ni lini Serikali itatambua umuhimu huo kwa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya kilimo hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kilimo ni moja ya sekta kubwa na muhimu katika uchumi wa Taifa letu na Serikali inatambua hili. Zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wetu wanategemea kilimo. Aidha, mchango wake kwenye Pato la Taifa sasa unakadiriwa kuwa takriban asilimia 26 na Taifa linategemea wakulima wetu kutulisha wote kwa chakula. Kwa kutambua umuhimu wa kilimo katika uchumi wa Taifa letu, Serikali imechukua na kusimamia hatua mbalimbali kuendeleza na kukuza kilimo nchini. Baadhi ya hatua hizi ni:-

(1) Serikali imeweka kilimo kikawa moja ya sekta za kupewa kipaumbele kwenye Bajeti ya 2007/2008 na kutengewa asilimia 6.30 ya bajeti ya Serikali.

(2) Kuimarisha Mfuko wa Dhamana wa Mauzo ya Nje (*ECGS*).

(3) Kuimarisha Mfuko wa Dhamana wa Kampuni Ndogo na za Kati (*SMECGS*).

(4) Kuimarisha Mfuko wa Dhamana kwa Mikopo ya Muda Mrefu.

(5) Kusimamia Mpango wa Maendeleo ya Kilimo (*ASDP*) unaotekelezwa chini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPS*).

(6) Kuamua, kuimarisha na kuirekebisha *TIB* kuwa Benki ya Maendeleo ya Taifa, ikiwa ni pamoja na kuiongezea mtaji. Mpaka hivi sasa *TIB* imekwishaongezewa mtaji wake kwa *Tshs 17bn/=* na Serikali imeamua kuwa itaongeza mtaji wa Benki hii kwa *Tshs. 50bn/=*. Hata hivyo, hili litafanyika kwa awamu na itakapoonekana kuwa mtaji mkubwa zaidi unahitajika Serikali itachukua hatua zinazofaa kuiwezesha *TIB* kufikia malengo yanayokusudiwa kama Benki ya Maendeleo ya Taifa ikiwa ni pamoja na kuchangia kwenye maendeleo ya kilimo.

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza, uamuzi wa kuongeza mtaji wa *TIB* kutoka Sh. *17bn/=* ilivyo sasa na kufikia Sh. *50bn/=* ni uamuzi uliofanyika mwaka 2004/2005. Serikali ya Awamu ya Nne mwaka 2006 ilisema na iliahidi kwamba itaongeza Sh. *50bn/=* katika mtaji wa *TIB* na mpaka leo ni miaka mitatu tangu Serikali itoe ahadi hiyo ya kuongeza mtaji wa *TIB*; je, ahadi hii isiyotekelezeka inatoa ishara gani kwa wananchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Arusha wameamua kuanzisha *Community Bank* ili kusaidia kutoa mikopo na huduma za fedha kwa wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo; je, Serikali inatoa tamko gani kusaidia mikopo ili kuanzisha Benki hiyo ya Wananchi katika Mkoa wa Arusha?

**NAIBU SPIKA:** Naomba ujibu swali la kwanza, la pili halihusiani na swali la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIA S. SUMARI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali inakiri kwamba mwaka 2005 iliahidi kuiongezea *TIB* mtaji wake wa hisa wa Serikali kwenye ile benki kwa kiasi cha Sh. 50bn/= na ni kweli vilevile kwamba mpaka sasa hivi Serikali imekwishaiongezea *TIB* mtaji wa hisa kwa Sh. 17bn/= . Tunakubali kwamba kutokana na ahadi hiyo bado Serikali ina deni la Sh. 33bn/= . Hilo nimesema kwamba Serikali itatimiza lakini ikwa awamu. Nataka niseme hivi katika mtaji wa *TIB*, Serikali haitegemei kwamba watasubiri hisa za Serikali tu maana mtaji wa benki una sura mbili au sehemu mbili; una mtaji wenyewe ambao ni wa hisa na pia una mtaji vilevile unaotokana na madeni ambayo yanatokana na kukopa kwa ile benki yenyewe.

Kwa hiyo, kama *TIB* ina nia kweli na tunajua ina nia ya kutimiza malengo yake ambayo yapo kwenye hati yake ya kuanzishwa, basi tunategemea kwamba pamoja na mchango wa Serikali wa Sh. 17bn/= mpaka sasa hivi *TIB* itakuwa ina pia miradi yake na mikopo kutoka sehemu zingine za mitaji. Kwa mfano, wanaweza kukopa kutoka *ADB*, Mashirika kama *FMO* ya Udachi na *PROPACO* ya Ufaransa. Hivyo, hili la Serikali ni sehemu moja tu ya mtaji wa *TIB* na menejimenti ya *TIB* isisubiri hizi fedha za Serikali ingawaje nataka kutamka hapa kwamba Serikali itatimiza ahadi yake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nasikitika kusema kwamba tumeanza kulegea jinsi ya kutumia kanuni ya maswali. Maswali yanayoulizwa ni marefu na maswali ya nyongeza yanakuwa hotuba. Tukifanya hivyo kwanza Bunge lenyewe litakuwa linazubaa maana sisi wote itabidi tukae tumsikilize huyo anayeuliza swali na anayejibu swali. Nina majibu ya Mawaziri wote hapa na nimesoma, mtu anatoa utangulizi *page* mbili, kumbe jibu ni mistari mitano tu. Sasa Waheshimiwa tukifanya hivi Bunge litakuwa *very boring* kwa sababu tutakuwa tunawasikiliza watu wanaotoa hotuba tu. Kwa hiyo, maswali yajibiwe kifupi sana na mimi nawaambia hizi habari mnazosimulia hawasikilizi, mtu anataka swali lake tu lijibiwe, hizi habari zote na utaalamu wote hawasikilizi, wanataka maswali yao yajibiwe, matokeo yake tunajirudia. Kwa hiyo, tunapoteza muda. (*Makofi*)

Wanaouliza maswali wanaanza kuhutubia, uliza swali lako, hotuba zako sisi hazituhusu. (*Makofi*)

Hicho ni Kifungu cha 39(1) kinachohusu Waheshimiwa Wabunge kuuliza maswali kwa kifupi. Kifungu cha 46(1), kinawataka Waheshimiwa Mawaziri kama wana majibu marefu wapeleke kwa maandishi. Sasa nilisema Wabunge msiongee ndani ya Bunge, ni Kifungu cha 66(3), kinamtaka Mbunge asiyezungumza akae kwa utulivu na

Wabunge wanaoondoka waondoke pia kwa staha na staha ni kuinama unapotoka na kuingia. Tunaendelea, Katibu!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umepita ndiyo maana nawaambieni kwamba hatuwezi kumaliza maswali kwa sababu ya urefu wa maswali na urefu wa majibu, swali moja limebaki kwa leo, kwa hiyo, tunaendelea na kazi ya leo.

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Matangazo!

**NAIBU SPIKA:** Matangazo kweli! Nimesahau wageni, matangazo ya wageni pia yanachukua muda lakini leo tuna bahati, wageni wote ni wa Mheshimiwa Missanga. Kwa hiyo, naomba wageni wote wa Mheshimiwa Missanga wasimame, maana yake ni Mwenyekiti Kata ya Mugaa, Mzee Shabani Selema; yuko Mwenyekiti Kata ya Mtuntu; Mwenyekiti Kata ya Sihuyu na Mwenyekiti Kata ya Misuga. Naomba Mheshimiwa Missanga upeleke kwenye ofisi wageni wako ili kusudi iweze kuwa *typed*, sisi miandiko mingine hatuwezi kuisoma, ndiyo utaratibu wetu. (*Kicheko*)

Halafu tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa ni Mkurugenzi wa Redio Uhuru, Ndugu Mikidadi Mahmoud; tuna mgeni mwingine mtangazaji wa Redio Uhuru, Vaileth Mzindakaya; mwingine ni Afisa Mawasiliano wa Redio Uhuru. Nilikuwa nashangaa wageni waliokaa kwenye *VIP* ya Spika, halafu siwajui kumbe walikuwa hawajaletwa hapa. Halafu tuna wanafunzi saba wa Chuo cha Biashara (*CBE*), naomba wasimame. Karibuni sana wageni wote mliopo! (*Makofi*)

Pia tuna matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa William Shellukindo, yeye anaomba Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuwa leo tarehe 14 kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika saa saba mchana katika Ukumbi Na. 227, ghorofa ya pili. Vilevile Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Haroub Masoud, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 14 saa tano asubuhi kutakuwa na kikao cha Kamati kwa ajili ya kuchambua Muswada. Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi Na. 231, ghorofa ya pili. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Jenista Mhagama amefiwa na baba mkwe wake, kwa hiyo, hayupo. Pia Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, yeye anaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane leo saa tano asubuhi katika Ukumbi Na. 428, Jengo la Utawala.

Kuna tangazo pia kwa Wabunge wote, hii inatokana na utawala Bungeni kwamba tunapenda kuwajulisha kuwa Kampuni ya Simu za Mikononi ya *Vodacom* itafanya maonyesho maalumu ya simu ya watu kwenye viwanja vya Bunge, nyuma ya Jengo la Utawala leo hii kuanzia saa tano hii. Waheshimiwa Wabunge mkipata nafasi mnakaribishwa kwenda kuona maonyesho hayo. Nilikuwa nimesahau kwa sababu muda uliliwa na maswali marefu na majibu marefu.

Sasa nadhani matangazo yamekwisha, Katibu!

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya UNESCO wa Mwaka 2008 (*The UNESCO National Commission Bill, 2008*)

(*Kusomwa Mara ya Pili*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Kuunda Tume ya Taifa ya UNESCO au *The UNESCO National Commission Bill, 2008*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto na Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. Tunawaombea kheri na baraka katika kazi zao na tunawakaribisha na kuwahakikishia ushirikiano wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omar Shaaban Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini kwa kujadili na kupitisha Muswada huu. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Omar Kwaangw,' kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Kamati hii ya Huduma za Jamii. Naomba pia niwapongeze wajumbe wote wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa kupata nafasi ya kuwa Wajumbe wa Kamati hii muhimu katika Bunge letu Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka mwanzo wa utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Elimu, Kamati hii imetoa mchango mkubwa katika kusimamia, kuelekeza na kushauri Wizara yangu ili kufanikisha utekelezaji wa mpango wetu wa sekta ya elimu. Ushirikiano wa Kamati hii unaonekana wazi katika mafanikio makubwa ambayo yamefikwa na nchi yetu katika sekta ya elimu. Ni matumaini yangu kuwa Kamati itaendelea kutoa ushauri na maelekezo katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi na ubora wa elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu tangu niteuliwe kuiongoza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba nichukue fursa hii ya kipekee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyonipa kwa kunitaua kuwa Waziri wa Sekta hii muhimu katika Taifa letu. Aidha, nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mwanga kwa kuendelea kuniunga mkono katika kazi ya kuleta maendeleo ya Wilaya yetu nikiwa Mbunge wao.

Madhumuni ya Muswada ninaouwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu ni kupendekeza kutungwa kwa Sheria ya Kuunda Tume ya Taifa ya UNESCO ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayojitegemea. Tume hiyo itakuwa na mamlaka kamili ya kusimamia, kuratibu na kutekeleza kazi za UNESCO katika Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania. Wadau watakaohusika ni pamoja na Wizara mbalimbali, taasisi za Serikali na zisizokuwa za Serikali, wataalamu mbalimbali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuundwa kwa Tume ya Taifa ya *UNESCO* inayojitegemea kunatokana na kuongezeka na kupanuka kwa shughuli za *UNESCO* katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu. Hivi sasa *UNESCO* inachangia sana katika sekta kuu tano ambazo ni elimu, sayansi asilia (*natural sciences*), sayansi ya jamii (*social sciences*), utamaduni, habari na mawasiliano. Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hizi na zingine zitakazoanzishwa, Serikali inaona umuhimu wa kipekee wa kuwa na Tume ya Taifa ya *UNESCO* inayojitegemea ambayo itakuwa na majukumu kama ifuatavyo:-

(1) Kusimamia na kuratibu shughuli za *UNESCO* kwa umakini zaidi ili kuongeza kasi ya maendeleo ya nchi yetu.

(2) Kuimarisha utekelezaji na usimamiaji wa shughuli katika Taifa letu ili wananchi wengi zaidi washirikishwe na wanufaike na shughuli za *UNESCO*.

(3) Kuimarisha ushirikiano kati ya Taifa letu na *UNESCO* pamoja na nchi wanachama wa Shirika la *UNESCO* ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umeambatana na marekebisho (*Schedule of Amendments*) katika baadhi ya vifungu na umegawanyika katika sehemu kuu nne kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza ya Muswada yenye Ibara za 1, 2 na 3 inapendekeza masharti juu ya mambo ya Utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria inayopendekezwa, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hiyo, matumizi yake na tafsiri ya maneno mbalimbali yanayotumika katika sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya pili ya Muswada yenye Ibara za 4 mpaka 12 inaainisha muundo wa Tume, majukumu na mamlaka ya Tume, uteuzi wa wajumbe wa Tume na muundo wa Sekretarieti ya Tume hiyo. Vilevile Muswada unaweka utaratibu wa kuunda Kamati za kitaalamu na kazi za Kamati hizo ambazo zinajumuisha kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Tume inayoundwa.

Sehemu ya tatu ya Muswada yenye Ibara za 13 hadi 15 inapendekeza masharti yanayohusu masuala ya fedha na rasilimali za Tume.

Sehemu ya nne ya Muswada yenye Ibara za 16 hadi 19, inapendekeza mambo mbalimbali yakiwemo makosa na adhabu, mamlaka ya Waziri kutoa maelekezo kwa Tume na mamlaka yake ya kutengeneza kanuni chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kupitia kwako, Waheshimiwa Wabunge waujadili Muswada huu na kisha kuukubali na kuupitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. OMAR S. KWAANGW’ – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ulioipa jukumu la kuufikiria Muswada wa Sheria ya kuundwa kwa Tume ya Taifa ya *UNESCO* (*The UNESCO National Commission Bill*, 2008).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kupata nafasi ya kusema hapa Bungeni baada ya kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Huduma za Jamii, naomba kwa heshima na kwa unyenyekevu mkubwa nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa namna ya pekee Waheshimiwa Wabunge, wajumbe wa Kamati hii kwa kunichagua kwa asilimia mia moja kuwa Mwenyekiti wa Kamati kwa kipindi kilichobaki cha uhai wa Bunge lako Tukufu. Heshima hii pia inatokana na wananchi wa Jimbo la Babati Mjini ambao wameendelea kuniunga mkono katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa Taifa letu na Jimbo la Babati Mjini. Ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo langu kwa imani, ushirikiano na upendo wao kwangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nimpongeze Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro ambaye nilikuwa Meneja wake wa kampeni kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto. Pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge, nawatakia heri na mafanikio katika kazi ya Ubunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono madhumuni ya Muswada wa Sheria ya Kuunda Tume ya *UNESCO* inayojitegemea ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia, kuratibu na kutekeleza kazi zote za *UNESCO* hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuundwa kwa Tume ya Taifa ya *UNESCO* inayojitegemea kunatokana na kuongezeka na kupanuka kwa shughuli za *UNESCO* hapa nchini katika kuchangia maendeleo yetu, hivyo, Kamati inakubali kuwa kuna umuhimu wa kuwa na chombo thabiti cha kupanga, kusimamia na kuratibu shughuli hizo kwa umakini zaidi ili kuleta maendeleo yaliyokusudiwa. Aidha, Kamati inatambua kuwa kuundwa kwa chombo hiki kisheria kunazingatia matakwa ya Hati Idhini (*charter*) ya *UNESCO* inayohusu uundwaji wa Tume za Taifa za *UNESCO*, kama ilivyopitishwa na kikao cha 20 cha Mkutano Mkuu wa *UNESCO* mwaka 1978.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Serikali ya nchi mwanachama ni kuunda Tume ya Taifa ya *UNESCO* yenye majukumu ya kuchangia katika juhudi za Wizara husika. Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali, pia Tume hii inahusisha wataalamu kutoka sekta mbalimbali ikiwemo sekta binafsi kushiriki katika shughuli za *UNESCO* kwa lengo la kuharakisha maendeleo ya wananchi kupitia sekta za elimu, sayansi asilia, teknolojia, sayansi ya jamii, utamaduni, habari na mawasiliano. Tunaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua hii muhimu katika kufanikisha lengo la kuharakisha maendeleo ya

wananchi kupitia sekta za elimu, sayansi asilia, teknolojia, sayansi ya jamii, utamaduni, habari na mawasiliano ambazo hupata msukumo wa maendeleo na ufadhili kutoka *UNESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhika kuwa kuanzishwa kwa Tume ya Taifa ya *UNESCO* inayojitegemea kutaweza kusimamia kwa karibu na kuratibu utekelezaji wa majukumu ya *UNESCO* hapa nchini na pia itakuwa kiungo na Ofisi ya mwakilishi wa kudumu wa *UNESCO* hapa nchini katika kutekeleza kazi zake na pia itafanikisha na kuharakisha maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekuwa ikinufaika kwa kupata ufadhili wa miradi mbalimbali kutoka *UNESCO* kwa ajili ya kuimarisha Elimu na Utamaduni kama ambavyo tumeweka kwenye jedwali miradi michache na nitajitahidi kutamka kwa ufupi kama ilivyoandikwa:-

Kwenye miradi ya *participation projects* kati ya mwaka 2005-2006 kulikuwa na miradi kama sita, *training culture of peace, Sub-regional Awareness Seminar of ASP Network in Lake Victoria Zone, Strengthening Veterinary Education through Information Technology, Upgrading of existing library and documentation Unit at Southern and Eastern Africa Mineral Centre SEAMIC, Capacity Building in Human Resources and Infrastructure*. Yote hii kwa kweli imefadhiliwa kwa dola za Kimarekani karibu 127,000.

Miradi mingine ambayo ni *Establishment of Information Technology Centers in Zanzibar, Procurement of Equipment and purchase of books, Capacity building at Mkwawa University College of Education, Conservation of Endangered Archives Zanzibar, Reviewing of National Science and Technology Policy of Tanzania 1996, Solar Lap-tops for Schools, Preparation of National Inventory of oral and intangible cultural heritage of ethnic societies in Tanzania Phase I, Proposal on SAQMEC III Project Zanzibar*, hii nayo ilifadhiliwa kwa Dola za Kimarekani 164,700.

Miradi mingine minne ni *Teachers Training Project within the Framework of Teaching Training initiatives for sub-Saharan Project, Roads to Independence, African Liberation Heritage Programme, Education Sector Management Information System, Science, Technology and innovation (STI) Review Project*, hii nayo imeleta Dola za Kimarekani milioni 1, 525,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na takwimu hizo chache Kamati yangu inaamini kuundwa kwa Tume ya *TANESCO* inayojitegemea kutakuwa chachu ya kuleta maendeleo na kuvuta fedha kutoka Umoja wa Mataifa na Wahisani wengine na kuharakisha maendeleo ya nchi yetu katika masuala ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, Kamati inatoa maoni yafuatayo kwa lengo la kuboresha na kufanikisha utekelezaji wa Sheria hii.

Sehemu ya kwanza: Katika ufafanuzi wa neno *Executive Secretary* Kamati inapendekeza maneno ya mwisho yawe *section 11 (2)* badala ya *section 9(2)* kwa kuwa kifungu hicho ndicho kinaongelea *Executive Secretary.*

Sehemu ya Pili: Kifungu cha 5(n) Kamati inapendekeza neno *'to'* lililopo mwanzo wa sentensi liondolewa kwa kuwa neno hilo halileti maana.

Kifungu cha 6(1)(b) Kamati inapendekeza kuwa wateuliwa wajumbe kumi badala ya tisa kutokana na umuhimu wao.

Kifungu cha 6(1)(ii) Kamati inapendekeza yatumike maneno *"Communication, Science and Technology"* badala ya maneno *"Higher Education Science and Technology"* kutokana na mabadiliko ya majina na majukumu ya Wizara kama ilivyotangazwa na Mheshimiwa Rais wakati wa mabadiliko ya Serikali.

Kifungu cha 6(1)(b)(vi) Kamati inapendekeza kuwa mwakilishi awe mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Waziri kutoka katika Chuo Kikuu chochote nchini na siyo lazima atoke Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ili kuweka uwakilishi mzuri katika Bodi, Kamati inapendekeza kuwa Waziri apewe uwezo wa kuteua wajumbe wawili, mmoja kutoka Tanzania Bara na mwingine kutoka Tanzania-Zanzibar. Kwa mantiki hiyo Kamati inapendekeza kuwa kiongezwe kifungu (d) ambacho kitampa uwezo Waziri kuteua wajumbe hao.

Kifungu cha 8(1) Kamati inapendekeza kuwa wajumbe wa kila Kamati wasizidi sita ili kuwa na wawakilishi muhimu kwenye Kamati za kitaaluma.

Kifungu cha 8(2)(a) Kamati inapendekeza kuwa kisomeke *"Ministry responsible for Science and Technology"* kufuatia mabadiliko ya Wizara za Serikali.

Kifungu cha 8(2)(b) Kamati inapendekeza kuwa kifungu hiki kiandikwe upya na kushirikisha Afisa Elimu Kiongozi na Idara inayohusika na Elimu ya Juu.

Kifungu cha 8(2)(d) Kamati inapendekeza kuwa mjumbe awe mwakilishi wa Chuo Kikuu chochote nchini chenye programu ya ualimu na asilazimike kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pekee.

Kifungu cha 8(3)(d) Kamati inapendekeza kuwa mwakilishi awe mtu atakayetoka Chuo Kikuu cha Serikali au Chuo Kikuu cha binafsi na isiwe Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pekee.

Kifungu cha 8(6)(d) Kamati inapendekeza kuwa wawakilishi wawe wawili, mmoja atoke Chuo Kikuu cha Serikali na mwingine Chuo Kikuu chochote cha binafsi.

Sehemu ya Nne: Kifungu 19(2)(c) Kamati inapendekeza kuwa yaongezeke maneno “*in conformity with the Public service Act*” mbele ya neno ‘*Secretariat*’ ili taratibu za uwajibikaji kwa utumishi ziweze kufuatwa kwa ufanisi.

Sehemu ya Jedwali: Kifungu cha 1(2) Kamati inapendekeza kuwa litumike neno ‘*may*’ badala ya ‘*shall*’ na kwamba baada ya neno ‘*re-appointment*’ yaongezwe maneno “*for a further term*” ili kumpa nafasi Waziri kufanya uteuzi kwa namna atakavyoona inafaa.

Kifungu cha 6(2) Kamati inapendekeza kuwa kifutwe kwenye jedwali hilo kwa kuwa kinaweka mazingira ya kukwepa kuwa na vikao vya kawaida vya Tume na hivyo kuhatarisha uhai na shuguli za Tume kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yote niliyoyataja na mengine yatakayoletwa na Mheshimiwa Waziri tulijadiliana kwa pamoja kati ya Wizara, Uongozi wa *UNESCO* – Taifa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hivyo naishukuru Serikali kwa kuleta Jedwali la Marekebisho ya Muswada huu linalozingatia maoni ya Kamati yangu kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutumia nafasi hii kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, (Mb.), na Manaibu wake Mheshimiwa Mwantumu Mahiza (Mb.) na Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, (Mb), kwa ushirikiano wao wakati Kamati ikifikiria Muswada wa Sheria hii.

Aidha, nawapongeza Wataalamu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wakiongozwa na Naibu Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji wa *UNESCO* Taifa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushirikiano wao na kwa kutoa majibu ya hoja za Wabunge kuhusu Muswada huu wa Sheria ya Kuunda Tume ya Taifa ya *UNESCO* ya mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa namna ya pekee nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kwa kumchagua Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima sasa naomba niwatambue wajumbe wapya uliowateua wa Kamati ya Huduma za Jamii walioteuliwa na Mheshimiwa Spika na ambao wamechambua Muswada wa Sheria hii ya Kuunda Tume ya Taifa ya *UNESCO* wa mwaka 2008 kwa kuwataja kwa majina:-

Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Prof. Feetham Banyikwa, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Omari Mzee,

Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Fatma Abdalla Tamim, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Janet B. Kahama na mimi Mheshimiwa Omari Kwaangw'. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa namna ya pekee napenda nitambue ushirikiano wa Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Kaimu Katibu wa Bunge, Ndugu Dr. Thomas D. Kasilillah. Vilevile nawapongeza Makatibu wa Kamati, Ndugu Theonest Ruhilabake na Hellen Mbeba kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi maoni haya kutolewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. MHE. SUSAN A. J. LYIMO-MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kuwa hapa ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani.

Pili, natoa shukrani zangu kwako wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya kuunda Tume ya UNESCO inayojitegemea ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (*The UNESCO National Commission Bill, 2008*), kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6) (c) na 86(6), Kanuni za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa niaba ya Kambi ya Upinzani natoa pongezi kwa Wabunge wapya wote kuwa pamoja nasi katika kazi ya kuwawakilisha wananchi.

Aidha, tunatoa salamu za rambi rambi kwa ndugu na jamaa wa familia za marehemu wote waliofariki katika migodi ya Mererani hivi karibuni. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amen!*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe pongezi nyingi kwa Waziri na Naibu Mawaziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na watendaji wote wa Tume ya UNESCO kwa kazi kubwa waliofanya hadi kufikia hatua hii ya uwasilishwaji wa Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu. Ni ukweli wa dhahiri kuwa Muswada huu utakuwa na manufaa mengi kwa Taifa letu hasa tukizingatia utandawazi na zaidi tuko katika Karne ya Sayansi na Technolojia. Tume hii kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri ni Tume inayohusika sana na Sayansi na Technolojia na tunajua ni jinsi gani nchi yetu iko nyuma katika fani hiyo. Ni kwa mantiki hiyo basi naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu huo na hivyo kuipa Tume mamlaka zaidi ili ijitegemee.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana nzima ya kutungwa kwa Sheria hii ni nzuri kabisa, na sisi kama Kambi ya Upinzani hatuna shida nayo, kwani Sheria hii itaifanya

Tume ya *UNESCO* kujitegemea na hivyo kuipa mamlaka ya kusimamia, kuratibu na kutekeleza shughuli za *UNESCO* nchini kwa kuzingatia taratibu za Serikali na *UNESCO*. Pamoja na umuhimu wa Sheria hii, tunamshauri Waziri husika aone umuhimu wa kuwapatia Wabunge wote semina kuhusu umuhimu wa kuelewa vizuri Tume hii ambayo tunaamini ina umuhimu mkubwa na maslahi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulipitiwa kwa kina na Kamati husika ambapo pia Kambi ya Upinzani iliridhika na marekebisho japo kuna baadhi ya vifungu ambavyo tunadhani bado vinatakiwa kuwekwa vizuri ili visitoe mkanganyiko katika utekelezaji wake. Hivyo basi, tunashauri Kifungu cha 3 cha Muswada kinachohusu maana au tafsiri ya maneno yatakayotumika katika Muswada huu, neno *UNESCO* ambalo ndio msingi wa Muswada huu halijatafsiriwa. Nina imani Wabunge na wadau wangependa kujua maana ya *UNESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 5, nanukuu: “*The Culture Technical Committee shall...*”, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi ni kwa nini isiwe “*The Culture and Information Technical Committee*” kwani hii ni Wizara moja na kwamba habari ni muhimu sana katika suala zima la kudumisha utamaduni wetu. Na hata ukiangalia Wajumbe wengine wanatoka Wizara ya Habari na Utamaduni Zanzibar.

Kifungu cha 11(2) kinaelezea uteuzi wa Katibu Mtendaji Mkuu (*Executive Secretary*). Kinasema atatumikia kwa miaka mitano, na atastahili kuteuliwa tena (*eligible for reappointment*). Lakini haisemi hii *eligibility* ya *reappointment* ni ya *terms* ngapi au ni *indefinite*?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 8(6)(d) pamoja na wajumbe wengine kinachosema kuwa katika wajumbe wa the *Communication Sector Technical Committee shall be composed of-* (d) *the Institute of Journalism and Mass communication, University of Dar es Salaam*. Tunaelewa kuwa Sekta ya Habari imepanuka sana na hivyo kuwa na Vyuo vingi vinavyotoa taaluma hii. Kutamka kuwa ni *University of Dar es Salaam* tu ni kuvinyima uwakilishi Vyuo vingine. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kifungu hiki kiondoe neno “*University of Dar es Salaam*” ili Waziri awe na uwanja mpana zaidi wa kuteua wawakilishi wengine wenye uwezo na pia italeta ushindani kwa Vyuo husika.

Kifungu cha 14(1)(a) cha Muswada kinaelezea vyanzo vya fedha za Tume ya *UNESCO* na kinaainisha vyanzo hivyo kama “*donation, grants, loans and gifts*”. Kambi ya Upinzani haina kipingamizi na vyanzo hivi ila ingependa kuelewa zaidi kwa mfano, zawadi au *gifts* zinawezaje kuwa chanzo cha mapato? Labda tungependa kujua zawadi hizo huja katika *forms* gani na kama si fedha *cash* wanazifanyaje kuwa chanzo cha mapato?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 15(2) ni changamoto kwa Tume kwani kinaelezea umuhimu wa kutayarisha ripoti zake na hivyo kumfanya Waziri mhusika

kuleta ripoti hii Bungeni. Napenda niipongeza Tume kwa uwazi huo na tunaamini watatekeleza haya.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 18 (5), nanukuu: “ *For the purpose of this section ‘former officer’ means any person employed as staff or employed of UNESCO.....*” Kifungu hiki kilipaswa kuondoka na kuwa kwenye sehemu ya kwanza ya tafsiri na si hapa kama kilivyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jedwali la Sheria kifungu cha (4) yaongezwe maneno “*but he will not have the right to vote.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kunisikiliza na Waheshimiwa Wabunge wote. Baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema sasa nimepata wasemaji watatu. Ninaye Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman ambaye pia ni Waziri wa Elimu katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hiyo, naanza na Mheshimiwa William Shellukindo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie kidogo Muswada huu wa Sheria ya Tume ya Taifa ya *UNESCO* wa Mwaka 2008.

Kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa jumla kwa kuleta Muswada huu. Tume hii ni kongwe na ni ya siku nyingi sana, kwa hiyo, imebaki tu kama Idara, Idara haikuwekewa misingi ya kuitekeleza Kisheria. Kwa hiyo, nazipongeza sana juhudi hizi za kuleta Sheria hii hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitakwenda kwenye Muswada moja kwa moja. Nakwenda kwenye Ibara ya 3, ningependa nipate ufafanuzi kidogo, pale inapotoa *interpretation* ya *Chairman*, kwamba “*Chairman*” means *Chairman of the Executive Committee and includes* kama imesahihishwa, lakini nimeangalia kwenye Jedwali la Marekebisho sikuona, kule ndani sikuona *Executive Committee*, nadhani ni *Chairman of the Commission*, nadhani lingetazamwa hilo.

Halafu kwenye ukurasa wa 4, Ibara ya 5(2)(e) imezungumzwa kwamba hapo kuna nafasi mbalimbali ambapo ni nafasi za kazi, nafasi ya *fellowship*, kazi za uelekezi na kadhalika. Sasa mimi napenda kueleza kwamba sisi Watanzania tumekuwa nyuma sana katika kwenda kufanya kazi kwenye Taasisi hizo. Sasa umefika wakati kwa kweli tujitahidi tuwe na Watanzania huko, na njia ya kufanya ni kwa hii Mamlaka inayoundwa sasa iwe inatangaza mara kwa mara kwenye magazeti nafasi zinazotokea kwenye Taasisi hii ili Watanzania wachukue nafasi ya kuziomba hizo, na vilevile waweze kwenda kufanya kazi hizo za uelekezi, *consultants* na kadhalika. Hiyo kazi kwa kweli ni muhimu ifanywe vinginevyo tutakuwa sisi ni watu wa kuchangia tu, lakini utakuta hatunufaiki na Taasisi hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 6 nina maoni yafuatavyo:- Sheria hii inahusu pande zote za Muungano, sasa katika uteuzi pale kidogo nadhani ni vizuri tuparekebishe. Ibara ya 6(1)(a) inasema “*the Chairman who shall be appointed by the President and the Vice Chairman who shall be appointed by the Minister subject to subsection three.*” Hapa ninasema kama hiki chombo ni cha pande mbili, sasa mmoja wa upande mmoja anateuliwa na Rais na mwingine atateuliwa na Waziri hapa si itakuwa tatizo hapa. Mimi nadhani wote hawa wangeteuliwa na Rais, na tuna Tume za namna hii ambazo zimefanyika hivyo, hatuoni kwa nini hiyo iwe tofauti. Kwa mfano, Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano ina *Chairman* na *Vice Chairman* na wote wameteuliwa na Rais. Lifikiriwe hilo tusilete migogoro ambayo haina msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara hiyo hiyo ya 6 ukurasa wa 6(4) pale panaposema kwamba katika uteuzi huo wa Rais pamoja na Waziri watazingatia mambo ya Elimu, uzoefu katika masuala mbalimbali na kadhalika, nadhani hapo tusingahau hili suala la jinsia. Jinsia nayo ingekuwa ni mojawapo ya vigezo hapa, tunakwenda kwenye Ubunge asilimia 50 kwa 50, sasa kwenye nafasi hizi nazo hatusemi iwe asilimia 50 kwa 50, lakini angalau jinsia ifikiriwe, na jinsia hatuzungumzii wanawake kwa kweli, tunazungumza na wanaume. Tusingependa kuona mahali pamoja ni akinamama tu ndiyo wanaongoza, wachanganywe hivyo ndivyo namna ya kuongoza Taasisi hizo na nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kwa kuwa nilisema nitakwenda kwenye Muswada wenyewe, nilikuwa nataka kusaidia tu, wakati mwingine ukiwa umekaa na kitu chako unaweza usikione, unaweza kutafuta kifungo ukadhani kimedondoka kumbe bado kipo. Nazungumzia Ibara ya 8 ambayo inanzia ukurasa 7 mpaka wa 8.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 8 Ibara ndogo ya 4(e) Mheshimiwa Waziri angetazama pale alipounganisha *a representative of Association of Public Universities and a representative of Association of Private Universities*. Ila *a representative of Association of Private Universities* ingekuwa (f) ikae peke yake isiunganishwe na hiyo. Nasema hivyo, kwa sababu Muswada huu ukitoka kama kuna .....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa William Shellukindo rudi hapo, nilikuwa sijafuatilia.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasema imeunganishwa hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ni ukurasa wa 8?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 8, Ibara ndogo 4(e) imeunganisha *a representative of Association of Public Universities and a representative of Association of Private Universities*, ile and ibakie, ‘a’ iondolewe pale halafu kifungu kile kiwekwe pale (f), halafu aweke ile ‘a’ iwe *representative*

zisiunganishwe. Nimeangalia huko kwingine kumekwenda vizuri tu, ni hiyo *omission* kidogo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niko kwenye ukurasa wa 11, Ibara ya 15 ninataka tu tuelewane tu na wenzangu maana hiki Kiingereza kuna shule nyingi za Kiingereza. Kuna *English*, kuna *English* ya Marekani, kuna *English* ya Tanzania. Lakini nadhani pale kwenye kifungu cha 15(1)(c) inapoanzia katikati kuna (i) hiyo. Sasa (ii)katika (c) inayosema *an account operation*, kidogo hapo naona tungerekebisha ile *an* ingeondolewa tu iwe *account of operations* na siyo *operation* moja, *operations* kwa sababu ni shughuli, zile *activities*.

Halafu inayofuata (iii) hiyo *again an audited accounts* iwe tu *audited accounts*. Halafu (iv) *an audited accounts again* nadhani ingekuwa *audited accounts* tu. Tatizo sisi wengine tulisoma zamani nadhani ndiyo matatizo tunayoyapata haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 17 ile sentensi inayosema “*may give specific or general direction*,” haiwezi kuwa moja kwa kweli, vinginevyo kisheria ukizibandika nyingi watauliza *what are therefore*, wewe si umesema *direction* moja tu ingawa kuwa ni *directions*. Kwa hiyo, hata hiyo sentensi pale mwisho wake ingekuwa *directions* badala ya kuiacha *direction* inakuwa kidogo haikamati zile *operations* kwa jumla; inakuwa kama ni moja tu inaelekea huko. Hii ni Sheria naomba ieleweke hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiona hivyo ni kwa sababu naenda kwa kufunga hizi kurasa. Ibara ya 19(2)(e) inaposema *prescribing anything which need to be prescribed, prescribing anything which need to be, I think needs to be prescribed*. Tungetengeneza lugha hiyo kidogo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi yangu yalikuwa hayo tu kwa sababu ilikuwa *stage* ya mwisho ya Muswada.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, nakushukuru sana kwa mchango wako, hayo ni mabadiliko madogo madogo. Nategemea Waziri ame-*take note*. Tunaendelea na Mheshimiwa Pindi Chana.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Muswada huu ambao unahusiana na masuala ya *United Nations Educational Scientific and Culture Organization (UNESCO)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taifa lolote tukitaka kujua Taifa litakuwa wapi miaka 10 au 20 ijayo ni muhimu sana tukaangalia watu wake. Taifa lolote linategemea sana rasilimali watu, na tunaposema rasilimali watu maana yake ni watu wenye uwezo, na tunaposema watu wenye uwezo maana yake ni watu walioelimika. Sasa katika Taifa kuelimika zipo taratibu mbalimbali za kuwawezesha watu hao wakaelimika. Tunakuwa na Wizara ya Elimu, tunakuwa na Taasisi mbalimbali ambazo zinashughulikia masuala ya elimu ikiwa ni pamoja na Tume hizi za Kimataifa yaani *UNESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwamba masuala haya ya Umoja wa Mataifa (*United Nations*) yalianzishwa mara baada ya Vita Kuu vya pili, ikaamuliwa kuweka mambo mengi sana katika Tume za Kimataifa, na katika Dunia hii ya leo tunazo Tume nyingi sana. Tunazo Tume zinazoshughulikia masuala ya Afya, Masuala ya Watoto ikiwa ni pamoja na masuala haya ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu sasa niipongeze Serikali kwa kuweza kutuletea Muswada huu ambao ni muhimu sana kwa Taifa letu, na sasa moja kwa moja niingie katika Muswada wenyewe ambao kwa kweli naupongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kifungu cha 6(1), kifungu kinaelezea *Composition of the Commission* yaani hiyo Tume itaunda na watu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kifungu cha 6 hebu sema vizuri.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6(1), kuna ile (a) na (b). Katika kifungu kile cha (b) kipengele cha 9 kinaeleza wawakilishi mbalimbali akiwepo mwakilishi kutoka *Umbrella NGO*. *Umbrella NGO* ni muhimu sana ikashiriki katika Tume hii, lakini nilikuwa na ushauri mdogo. Chombo hiki kinachoitwa *Umbrella Non Governmental Organization*, yaani Tanzania *Non Governmental Organization* ni *TANGO* chenyewe kazi yake ni ku-*co-ordinate NGOs* zingine mbalimbali. Hivyo, mimi nilikuwa nashauri hii *Umbrella NGO* yenyewe ishauri ni mwakilishi yupi atakayefaa kuwepo kwenye ile Tume, kama kazi ya *Umbrella* ni *co-ordinate*; na kwa kuwa *NGO* zote zinakuwa chini ya *Umbrella* zinazohusiana na masuala ya Elimu, Watoto, *HIV*, Wanawake, hivyo, hii *Umbrella* itakuwa inajua ni Taasisi ipi inayoshughulikia masuala ya elimu ili kuweza kupata uwakilishi huo. Kwa hiyo, huo ndiyo ushauri wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendeleo Ibara ya hiyo hiyo sijaona *beneficiary* wa masuala ya elimu, na ninapozungumzia *beneficiary* katika kifungu hiki ninamaanisha wadau ambao ni wanafunzi, naona wengi wanatoka Wizara mbalimbali. Kwa hiyo, nadhani ipo haja ya kuwa na *beneficiary*. Kwa hiyo, ningepomba sana Wizara iangalie kama wataweza kumchukua mwakilishi yeyote kutoka *one of the Universities* ambaye anashughulikia masuala ya Sayansi na *Culture*, awe ni mmoja wa Wajumbe wa Tume hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema msemaji aliyepita Muswada huu umezingatia sana Wizara mbalimbali husika yaani wale wadau wa masuala ya elimu. Lakini masuala ya jinsia sijaona sehemu yoyote ambapo yamezingatiwa. Hivyo, ni ushauri wangu kwamba masuala ya jinsia katika kuwachagua wale Wajumbe wa Kamati mbalimbali ambazo zitakuwepo humu ni muhimu sana yakazingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kifungu cha 6 kwenye *schedule under section 6, 5* kule mwisho kabisa wa Muswada huu kwenye *schedule* kinazungumzia kuhusu *decisional of the Commission*. Kinasema kwamba kutakuwa na *decision of the Commission*. Sasa maamuzi yale yanaruhusu endapo mjumbe mmoja akiwa hayupo ana

haki ya kutuma mwakilishi. Kwa hiyo, akimtuma mwakilishi ni muhimu tukumbuke kwamba yule mwakilishi atakuwa hana haki ya kupiga kura, ila atakuwa na haki ya kutoa maoni mbalimbali.

Kifungu cha 12 huko huko kwenye *schedule* kinazungumzia kuhusu *sensation of membership*. Kwamba ni wakati gani mjumbe wa Tume hii ya *UNESCO* atakuwa amekoma kuwa mjumbe na ziko sababu mbalimbali ambazo kimsingi zimewekwa, endapo atakufa, atakuwa na matatizo ya akili. Sasa naomba kiongezwe kifungu cha (f) na kifungu hicho kitamke kuwa: “endapo atakwenda kinyume na *regulations...*” kwa sababu kwa mujibu wa Tume hii Waziri atakuwa na uwezo wa kuweka *regulations* ambazo zita-*operate internal operations* za shughuli za Tume. Kwa hiyo, endapo mjumbe yeyote au mtu yeyote mhusika atakwenda kinyume na zile *regulations or principles or bye-laws regarding this bill* napo atakoma kuwa mjumbe. Kifungu cha 1 kwenye *schedule* sehemu ya 2 kinaelezea *tenure of office* na kimeelezea kwamba Mwenyekiti atakuwa na haki ya kuchaguliwa tena (*re-appointed*). Kifungu cha 1 *part II* pale kwenye neno la mwisho kinasema, “*shall be eligible for re-appointment*”, naomba liongezwe neno “*once*” kama lilivyowekwa sehemu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni hayo naomba kuunga mkono hoja endapo maoni yangu yatazingatiwa. Ahsante sana.

**MHE. ALI HAROON SULEIMAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii muhimu kwangu mimi na kwa manufaa ya elimu hapa Tanzania.

Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Waziri kwa kuwasilisha Muswada huu na kwa umuhimu wake katika nchi yetu. Lakini la pili nimshukuru aliyekuwa Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Msolla, (Mb.), kwa sababu kazi hii tulishirikiana vizuri sana hapo awali na hadi kufika hapa ilipofika, naomba kupitia kwako nimshukuru sana pamoja na Naibu wake. Baada ya kusema hayo, nina maoni mawili, matatu na ushauri na ningeomba Mheshimiwa Waziri akauzingatia katika suala zima la kuufanya Muswada huu uwe bora. Naepuka sana kutumia neno kuboresha kwa sababu huwa silipendi sana, lakini kuufanya uwe bora zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Shellukindo alizungumza suala la uteuzi wa Mwenyekiti kufanywa na Rais, mimi sina tatizo na hilo. Lakini Muswada unasema kwamba endapo Mwenyekiti atatoka upande mmoja wa Muungano basi Makamu wake atatoka sehemu nyingine, hilo halina tatizo. Lakini ushauri wangu wala sina matatizo kwamba Makamu Mwenyekiti kuteuliwa na Waziri. Lakini endapo Mwenyekiti ameteuliwa ametoka upande wa Tanzania Bara *on merit* basi Makamu Mwenyekiti atateuliwa na Waziri baada ya Waziri anayehusika na *UNESCO* kushauriana na Waziri mwenzake anayehusika na *UNESCO* Zanzibar. Nadhani hiyo italeti sura nzuri zaidi iwepo kwenye sheria ione kane wazi wazi, hapa kidogo imejifungafunga, hapa atateuliwa na Rais. Rais wa Jamhuri atamteua Mwenyekiti sawa, anaweza akamteua kutoka upande mmoja wa Muungano. Akimteua kutoka Zanzibar basi Waziri anayehusika na *UNESCO* upande wa Tanzania Bara huku atakuwa anafanya uteuzi wa Makamu Mwenyekiti. Lakini endapo anatoka

katika Jamhuri ya Muungano upande wa Bara basi yule Naibu Waziri atakapokuwa anamteua basi afanye *consultation* na Waziri mwenzake anayehusiana na mambo ya elimu au *UNESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kifungu cha 8 sehemu (b) pale “*Education Technical Committee shall be composed of member appointed from...*” Hakuna matatizo imejieleza vizuri. Ningesauri hapa na imeelezwa vizuri hapa:- (a) “*The Ministry responsible for Communication and Science and Technology Department of Higher Education;* (b) *The Ministry responsible for Education and Vocational Training*”. Hii haikujieleza anatoka sehemu gani. (c) *The Ministry responsible for Education and Vocational Training in Zanzibar*. Mimi nadhani ingeachwa kama ilivyoachwa hapo (b) isiwekwe “*Office for Commissioner for Education*”.

Mimi nadhani Waziri mwenyewe aachiwe, atateua mtu ambaye anajua hana uzoefu wa mambo haya ya elimu na sayansi nadhani itakuwa ni vizuri zaidi kuliko kuweka “*Office of The Commissioner*” pale moja kwa moja. Kwa sababu hata hapa (b) haikuwekwa “*Office ya Commissioner*” au “*Chief Education Officer*” imeachwa tu “*Ministry of Education and Vocational Training*”. Halafu (d) kuna “*The Dar es Salaam University College*” yaani atoke mjumbe mmoja kutoka *Dar es Salaam University College*. Mimi ningesauri basi kiongezwe kifungu cha (e), huku kuna (e) ambayo inasema *UNESCO National Commission* lakini kiongezwe cha (e) kwanza kabla hakijaja cha (e) chenyewe, *The State University of Zanzibar* vile vile iingizwe hapa. Kwa sababu hayo ni masuala ya *Higher Education* na kule Zanzibar kwa vile tunacho Chuo Kikuu chetu cha Taifa basi ni vyema nikashauri kwamba hilo likawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningesauri na ninavyoyakumbuka katika makubaliano ya awali kwenye *Deputy Executive Secretaries* hawa, tulikubaliana kwamba kama utaratibu wa Mwenyekiti unaotumika basi na utaratibu wa Katibu Mtendaji utumike ule ule, kwamba hapa sasa pameongezeka *two Deputy Executive Secretaries*. Makubaliano ya awali ninavyokumbuka tulipokuwa tumekaa na Profesa Msolla na hata Waziri aliyetangulia Dr. Pius Ng’wandu ilikuwa kwamba akitokea Katibu Mtendaji kutoka upande mmoja wa Muungano basi *deputy* atokee upande mwingine wa Muungano, ni mmoja tu hakuna haja ya kuweka wawili. Ni hivi karibuni nimezungumza na Mheshimiwa Spika, nimemwomba vilevile aniingize kwenye Kamati hii nadhani kama ningekuwemo kwenye Kamati hayo mengine nisingekuwa na haja ya kuyasema hapa leo. Lakini imebidi nifanye hivyo kwa sababu sikupata bahati kuwemo kwenye Kamati. Unajua hii dhamana ya Uwaziri inanifanya wakati mwingine nisiwemo kwenye Kamati, lakini nikija hapa mimi nakuwa ni Mbunge, nadhani ingefaa niwemo kwenye Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoshauri ni kwamba abakie *Deputy Executive Secretary* mmoja tu ili tusi-*complicate* mambo. Kama ya *Chairperson* vilevile kule anatoka mmoja huku na upande huu wa Katibu Mtendaji iwe ni hivyo hivyo. *Otherwise* sina matatizo na nampongeza sana marekebisho hayo naomba yazingatiwe kwa umakini

sana kwa faida ya maendeleo ya elimu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa kama nilivyosema watu wenyewe waliokuwa wanachangia walikuwa watatu tu. Tunapochangia Miswada Mawaziri wengine hawazuiwi kuchangia na hasa kama walikuwa na nafasi nzuri zaidi kabla ya wakati huu. Naona inakuwa lazima Mbunge hata Mawaziri wanaweza kuchangia kama wachangiaji. Kama hatuna mtu mwingine basi naona nitamwita Naibu Waziri mmojawapo au hapana tunaendelea kwa sababu mabadiliko sio makubwa.

### MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono Muswada huu upitishwe hasa kwa vile ulivyowasilishwa na Wizara vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara isimamie vizuri na elimu itolewa ili tuweze kutumia Muswada wa Sheria hii kwa faida ya Tanzania. Tume hii izingatie maslahi na iondoshe vikwazo vidogo vidogo iweze kuleta malengo yaliyokusudiwa na (Membe) au Wajumbe izingatie uwiano.

Kwa niaba ya wananchi wa Magogoni naunga mkono hoja ahsante.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Salaam aleikum!

Nakupongeza kwa kuwasilisha Muswada huu wa *UNESCO*. Nilikuwa na mchango mdogo ufuatao:-

(1) Katika kipengele 8(3) – *The Natural Science Technical Committee*.

(2) Natambua *any technical committee needs learned people*, ila mantiki ya kuweka *membership* kwa watu  $\frac{3}{4}$  wa Vyuo Vikuu napata shida kuelewa. Kwani natambua kuwa kuna Taasisi, na *very successful private organisations* ambazo *membership* yao ingesaidia sana, *rather than one focus of donors, though I also respect them. What do you say about this?*

(3) *Part IV (17) General Provisions:- “The Minister gets all the advise* kutoka kwenye Tume hii, kwa hiyo, nashindwa kuelewa *rationale* ya kifungu hiki, hasa pale inaposema *“and the commission shall give effect to such direction”*, kwani *my belief the valuable information* inatokana na Tume, *how again does the Minister directs? Please clarify.*

(4) *General concern:-* (a) Kwa sababu Kitengo cha *UNESCO* kimekuwepo kwa muda mrefu, lakini ni watu wachache sana wanaojua. Kabla ya uundwaji wa Tume hii, kuna ripoti yoyote iliyopo ambayo inaonyesha mafanikio na matatizo na mapungufu

yaliyokuwepo. Kwani hii Tume isije ikaanza ku-*invest the wheel*, kwani mengine ya majukumu yalikuwa yanaendeshwa kwa kiwango *of course* si kikubwa, kama ambavyo Tume itafanya, wengine tumefanya kazi na *UNESCO*, *there are a lot of things to be learnt and strengthened. Is there any information available, and has it been made use of?* (b) *Lastly, don't forget to change the name of Ministry*, isomeke Waziri Maghembe na si Msolla. Hongera *and thanks*.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze kwa muswada huu.

*S.6 (i) (ix) Composition of the Commission (ix)* imesema *the umbrella NGO* chombo hiki kina wajumbe wachache sana na wanahitajika sehemu nyingi, nashauri *umbrella NGO* yenyewe ipendekeze jina la mhusika kutoka *NGO* inayohusika na masuala ya Elimu. Kwa mfano, Hakielimu na kadhalika kazi ya *umbrella NGO* ni ku-*coordinate* tu. *Otherwise* kutokuwa na *conflict of interest* yenyewe *umbrella NGO* ikiwa inaenda kuwakilisha sehemu mbalimbali.

Pili, katika wajumbe wa *Commission* waongezeke wanafunzi ambao ndio *beneficiary* wa elimu. Kwa mfano, *President* wa Chuo cha Sayansi *beneficiary* yeyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati nyingi za Muswada huu *Gender* haijazingatiwa, nashauri izingatiwe.

*S.6 Under section 6(s) Decision of the Commission. Right to vote: "Those who are not members of the Commission shall not have the right to vote". S.4 i.e. if a person is nominated by another person from his organ to represent him in the meeting he shall have no right to vote.*

*S. 12 Cessation of membership iongezwe (f) goes against the Bye-laws or principles or Regulations The UNESCO National Commission Act, 2008.*

*S 1 (1) kwenye Schedule, Tenure of Office* baada ya neno *eligible for re-appointment* liongezwe neno *once*.

Nashauri Tume ya *UNESCO* iwe na uwezo wa kutunga *bye-laws* zake kwa ajili ya shughuli zake za ndani (*operational activities*).

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya kuunda Tume ya Taifa ya *UNESCO*.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza ili kujibu baadhi ya mazungumzo na michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge sasa hivi kuhusiana na Muswada huu wa *National Commission of Tanzania*.

Awali ya yote naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliojitokeza kuchangia Muswada huu. Nianze na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii ambaye tumefanya naye kazi kwa karibu sana ili kuufikisha Muswada huu katika hali ambayo sasa hivi upo. Bila kupitia vipengele alivyovizungumza lakini karibu yote aliyoyagusia katika marekebisho yako katika *Schedule of Amendments* na yatafanyiwa kazi kama tulivyoshauriana katika Kamati na kama alivyoyataja hapa kwa sababu tuliona umuhimu wa kufanya marekebisho haya. Kwa hiyo, mkiangalia *Schedule of Amendments* vipengele vingi alivyovizungumza Mwenyekiti wa Kamati vimekwishafanyiwa kazi pamoja na hizo *projects*.

La pili, ni hii tafsiri ya neno *UNESCO* ambalo limezungumzwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Lakini pia nikubaliane naye kwamba kama itaonekana kuna ulazima wa kutoa tafsiri basi itolewe wakati wa semina ambayo imeombwa, na sisi tunaona kuna umuhimu wa kuwapa Waheshimiwa Wabunge semina hii kama itaonekana inafaa na tuna nafasi ya kufanya hivyo ili kuwapa Wabunge nafasi ya kuifahamu *UNESCO*. Kutokuwa na wengi kuchangia hapa leo inaonyesha kwamba si Wabunge wengi wako *familiar* na *Commission* hii ya *UNESCO*. Wengi wangukuwa na ufahamu na *UNESCO* nafikiri wangeweza kuchangia. Kwa hiyo, hili ombi nafikiri ni muhimu Mheshimiwa Waziri atalisemea zaidi lakini nafikiri pale ndiyo itakuwa nafasi muafaka ya kutoa zaidi ufafanuzi wa *UNESCO* hasa shughuli zake katika Wizara mbalimbali. Kwa sababu *UNESCO* ni suala mtambuka kama tunavyoona kwamba tunashughulika na utamaduni, zikiwemo sayansi za jamii na *natural sciences*. Kwa hiyo, ni suala mtambuka na ni vizuri lieleweke na litawagusa Waheshimiwa Wabunge kwenye majimbo yenu kwa namna moja au nyingine yakiwemo na masuala ya utamaduni.

Mheshimiwa Shellukindo pia amezungumzia masahihisho ambayo mengi tumekwishayafanyia kazi. Kuhusiana na suala la kazi kutangazwa kwenye magazeti ili wazalendo waombe nafikiri hii ni moja ya shughuli sasa hivi ya Serikali kwamba ukiangalia suala zima la Jumuiya ya Afrika Mashariki na ajira kwa kweli tunajitahidi kwamba Watanzania wasibaki nyuma. Kwa hiyo, mahali pale ambapo Watanzania kiutaalamu wanaweza kupatikana hizi kazi kwa kweli sio kwa ajili ya wataalamu wa nje, hasa katika *Technical Committee* tutajitahidi kuhakikisha kwamba Watanzania ndio wahusike zaidi katika hizi *Technical Committees za committee* nyingi katika *UNESCO*.

Suala la *gender* kuhusiana na alivyozungumza Mheshimiwa Pindi Chana kwa maandishi na pia kwa kuzungumza, lipo, kuna mjumbe ambaye anatoka kwenye *Women Affairs*. Mimi nafikiri ukishazungumzia *Women Affairs* maana nafikiri wengi wanapodai *gender* haikufanyiwa kazi wana maana ya mwanamke kuonekana katika uteuzi. Kwa hiyo, pamoja na wataalamu kwamba elimu itazingatiwa, uzoefu utazingatiwa na utaalamu utazingatiwa, ni pamoja na kwamba suala la *gender* pia litazingatiwa. Kwa hiyo, unapoteua mtu ambaye ana utaalamu, mtu ambaye ana elimu ya kutosha hatutaacha suala la *gender*. Tutachukua *specifically* mtu ambaye anatoka kwenye masuala ya wanawake. Ndiyo maana yametajwa pale *Women Affairs*, lakini tunashukuru ni angalizo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii kwa kuwa masuala mengi yalikuwa yanazungumzwa, naomba niishie hapo. Ahsante sana na naunga hoja mkono hoja hii.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikushukuru sana kwa jinsi ambavyo umeendesha shughuli ya Muswada huu kwa *efficiency* ya hali ya juu na kwa haraka iwezekanavyo. Napenda sana kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia katika Muswada huu kwa kuonyesha ni jinsi gani ambavyo wameusoma kwa makini na kutoa mawazo ambayo karibu yote tunayakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza basi niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wameongea na kuchangia kwenye Muswada huu. Wa kwanza ni Mheshimiwa Omar Kwaangw, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii. Wa pili ni Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na wa tatu ni Mheshimiwa William Shellukindo, wa nne ni Mheshimiwa Pindi Chana na wa tano Mheshimiwa Ali Haroon Suleiman, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wa mwisho kwa kusema hapa Bungeni ni Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mbunge wa Magogoni, Zanzibar. Katika kukusanya makaratasi hapa Mheshimiwa Pindi Chana pia alileta mapendekezo kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Muswada huu umeshirikisha sana Waheshimiwa Wabunge na hasa Kamati katika kuujadili na kuhakikisha kwamba unaingia ndani ya Bunge ukiwa tayari. Kwa hiyo, mapendekezo ambayo yameletwa ni mapendekezo ambayo madogo madogo na kwa kweli mapendekezo ambayo yameletwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii na yale ambayo yameletwa na Mheshimiwa Msemaji wa Upinzani ni mapendekezo ya kimsingi na mapendekezo hayo tutayajumuisha katika Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shellukindo amesoma Muswada huu na kuhakikisha kwamba kila koma iko mahali pake na kila *full stop* iko mahali pake. Tunamshukuru sana na mapendekezo ambayo ameyatoa kama mlivyoyasikia hapa yalikuwa ni mazuri sana na tutayajumuisha katika Jedwali hili la Marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeyapokea mapendekezo ya Mheshimiwa Pindi Chana na kwa ujumla ni mapendekezo mazuri. Ningependa tu kusema kwamba tunapofanya *reference* kwa *gender* ni kwa maana ya mume au ni mke na kama tunaielewa kwa maana hiyo kwamba ni wanaume na wanawake basi tutazingatia hizo katika uteuzi wa wajumbe katika Kamati kwenye Bodi yenyewe. Na katika Kamati ambazo zimeundwa Kamati za Kiteknolojia tutahakikisha kwamba uteuzi huo unakaribia karibia yale ambayo tunaielewana kimsingi kwamba yakaribiane karibiane kuwa *fifty*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine muhimu sana yaliyoelezwa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni ya msingi na nimezingatia hasa marekebisho yale ya *section 6(1)(a)*.

Tumeyazingatia na tumezingatia pia marekebisho yale ya kuwa na Naibu Katibu Mtendaji wa Tume kuwa mmoja na kwamba tunarekebisha, Waandishi wa Sheria wanashughulikia ili iwe kama Katibu Mtendaji anatoka sehemu moja ya Muungano basi Naibu Katibu atoke sehemu nyingine ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Gaudencia Mgosi Kabaka ambaye amejibu kwa kweli zile hoja zingine ambazo na zenyewe sio nyingi. Nisisitize tu kwamba tutafanya semina ya Wabunge wote ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuielewa Tume hii ya *UNESCO*. Baada ya kusema haya naomba sana Waheshimiwa Wabunge muupitishie Muswada huu ili uwe sheria na Tume hii ianzishwe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge tutakapofika kupitia kifungu kwa kifungu katika Muswada huu kuna marekebisho ambayo tayari jedwali lake limesambazwa. Kuna marekebisho mengine yamefanywa na Wabunge wakati wa mjadala. Sasa tunapofika kifungu kile kama Waziri anaafiki yale marekebisho atasimama na kusema hasa yale ambayo hayako kwenye jedwali. Kama Waziri hakusema yule aliyehusika atasimama na kutueleza hayo halafu tutazungumza kama yaingie ama sivyo. Kwa hiyo, hivyo ndivyo itakavyofanywa, ingekuwa wameweza kuleta jedwali ingekuwa hivyo. Kwa hiyo, hivi ndivyo itakavyokuwa, Mawaziri mjiandae na Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wameonyesha kupendekeza jambo fulani libadilike pia watasimama wakati tukiingia kifungu kwa kifungu. Hiyo ndiyo kazi ya wakati wa Kamati ya Bunge Zima.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

*(Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti)*

### **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya UNESCO wa Mwaka 2008**  
*(The UNESCO National Commission Bill, 2008)*

Ibara ya 1

Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu tuwe na uhakika kwa sababu kuna marekebisho kwenye *Schedule of Amendments* lakini kuna lile ambalo nilidokeza pale kwamba mstari wa 2 unasema: “*Chairman means Chairman of the Executive Committee.*” Nilikuwa nasema nadhani *Commissioner* kwa sababu nimeangalia sikuona *Executive Committee* hapo. Tulikuwa tuelewane na Waziri kwamba kama ni hilo basi sina neno.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue fursa hii nimtambue Mheshimiwa Beatrice Shellukindo kwa mchango wake wa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, analolisema Mheshimiwa William Shellukindo ni sawa kwamba ni “*Chairman of the Commission*”. Kwa hiyo, tutarekebisha pale, badala ya *Executive Committee* tutaweka “*Commission*”.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 4

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilikuwa nimedokeza, na sikuona kwenye *Schedule of Amendments* kuhusu....! Samahani ile ni 6, hii nyingine imepokelewa tu nafasi kutangazwa. Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 6

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hapo nilisema unaposhughulikia mambo ya pande mbili basi kama ni “*Chairman*” au “*Vice Chairman*” inabidi wote hao wateuliwe na mtu mmoja kama ni Waziri au ni Rais. Hapa naona kuna mmoja *Chairman* anateuliwa na Rais lakini *Vice Chairman* anateuliwa na Waziri.

Nilikuwa nadhani ni vizuri kwa sababu tuna mifano ya Taasisi hizi za Muungano ambazo uteuzi wake unakwenda, na nimefurahi kwamba Waziri wakati anatoa maelezo

kuhusu Katibu Mtendaji alisema basi Naibu Katibu Mtendaji atatoka upande mwingine. Sasa ile *appointing authority* ya hawa watu wa pande mbili inabidi iwe ni ya mtu mmoja japokuwa mapendekezo yanatoka kwenye yale maeneo yanayohusika. Ahsante sana.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikiliza sana mawazo na mawazo aliyotoa Mheshimiwa William Shellukindo na makubaliano yale ambayo awali Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia *UNESCO* Zanzibar na Mheshimiwa Waziri anayeshughulikia *UNESCO* katika Baraza la Mawaziri la Muungano, napendekeza kwamba tuchukue yale makubaliano ambayo yalifikiwa isipokuwa katika eneo lile la *Section 6(1)(a)* tuongeze kwamba itafanywa “*in consultation with a Minister responsible for education in Zanzibar*”.

**MWENYEKITI:** Hoja hapa ni kwamba, “*The Chairman who shall be appointed by the President and Vice Chairman who shall be appointed by the Minister subject to sub-section 3. Pendekezo linalotolewa hapa kwamba both of these people should be appointed by one authority. What do you say about it?*”

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *finally appointment* hii itafanywa na Serikali na hapo awali katika Miswada kama hii ambayo inahusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kunakuwa na mawasiliano na majadiliano ya kina ambayo pande zote mbili wanakubaliana kwamba wafanyeje.

Sasa katika hili makubaliano yalikuwa kwamba Makamu Mwenyekiti atachaguliwa na Waziri anayeshughulikia masuala ya *UNESCO* kwa mashauriano na Waziri wa Elimu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba tubakie na makubaliano hayo ambayo yamekubaliwa na Wizara zote mbili.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na makubaliano hayo mimi kama Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania napenda kutoa ushauri kwamba ni vizuri tukaweka mambo yawe sawa. Mapendekezo yanapendekezwa na ule upande unaohusika lakini hii ni asasi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kiongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Rais, sasa ni vizuri hiyo ijitokeze wapendekeze kila kitu, kwenye hizi Tume nyingine mbona iko hivyo.

Mimi ni Mwenyekiti wa Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano na Makamu anatoka Zanzibar, wote tumeteuliwa na Rais lakini mapendekezo hayakutoka kila upande. Mimi nadhani kusiwe na *double standard*, tutakuja kuulizwa na wananchi kwa nini tunafanya vitu kama hivi? Naomba haya yawe kwenye *Hansard* lakini wanaweza wakaendelea na haya ambayo wameyakubali ili tusivuruge makubaliano isipokuwa ijitokeze kwenye *hansard* kwa kumbukumbu ya baadaye.

**MWENYEKITI:** Msiponisaidia mimi kwa nini achaguliwe na Rais au kwa nini aendelee kuchaguliwa na Waziri kama inavyosema hii ya 50? Mheshimiwa Marmo!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Mheshimiwa Shellukindo ni mazuri, lakini ametambua kwamba Kamisheni ya *UNESCO* ni tofauti kabisa na Tume ya Pamoja ya Fedha. Tume ya Pamoja ya Fedha inaanzishwa kwa masharti ya Katiba. Kwa hiyo, mashauriano yote yanafanywa kwa ngazi hiyo. Sasa Kamisheni ya *UNESCO* inaanzishwa na Sheria ya Bunge ambayo inakuwa *administered* na Waziri. Kwa hiyo, mawasiliano katika ngazi hii yanakuwa mazuri zaidi, yanakuwa baina ya Waziri na Waziri na ndicho kinachopendekezwa hapa na hatimaye dhamira anayoelezea Mheshimiwa Shellukindo itatekelezwa kwa sababu tunataka angalau kuwe na uwakilishi wa upande mmoja wa Muungano.

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 9

Ibara ya 10

Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 12

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 13

Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

**MHE. WILLIAM D. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu niwe na uhakika kwamba lile nililodokeza pale Waziri naye amelichukua vizuri kwenye 15 (i) ile (c) kuna moja imefutwa (iii) ni sawa? Lakini kwenye ile (i) (a) ilisema kwamba pale ingekuwa *account* tuondoe ile *an iwe account of operations during the year* maana yake ni shughuli nyingi isiwe ni *operation* moja kama inakubalika. Halafu ile (iv) *an audited accounts* si lugha ambayo imekaa vizuri, ile *any* iondolewe lakini ibaki *audited accounts*. Ni hilo tu.

**MWENYEKITI:** Sawa kabisa.

**MHE. ATHUMAN S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa sikuchangia huko mwanzo katika kifungu cha 15 (ii) naomba nimshauri Waziri tu kwamba hivi kilivyokaa kinaacha mwanya wa Tume kutokupeleka taarifa kwa Waziri mapema.

Kwa hiyo, nashauri maneno yasomeke hivi: *“the annual reports of the Commission and the auditor’s reports shall be forwarded to the Minister within kama miezi miwili au mitatu halafu iendelee kwamba who shall as soon as may be practicable lay the reports before the National Assembly.* Bila kuweka kipindi maalumu baada ya mwaka kumalizika Tume inaweza ikachelewesha ripoti ikawa haina maana, ahsante.

**MWENYEKITI:** Umesikia pendekezo hilo?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kipindi cha miezi sita kitawapa nafasi kukamilisha kazi hiyo.

**MWENYEKITI:** Sijui maana yake kuna Sheria nyingine zinazosema kwamba hesabu zitawasilishwa kwa Waziri baada ya kufungwa katika kipindi fulani halafu zinawasilishwa Bungeni baada ya kipindi kingine. Sasa nisingependa useme wewe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE NA URATIBU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, *audit exercise* inapokamilika baada ya miezi mitatu lazima vitabu hivi viwasilishwe kwa Waziri na Waziri atawasilisha Bungeni haraka iwezekanavyo. Kwa hiyo, kwa taratibu ni *three months after audit exercises*.

**MWENYEKITI:** Nafahamu kwenye Sheria tuliyotunga ama ipo kwenye *Parastatal Accounts Committee au something like that*. Ipo ambayo ina-stipulate kabisa kwamba mkifunga hesabu Waziri anapewa hesabu na baada ya miezi kadhaa Waziri anawasilisha Bungeni. Nadhani tutumie Sheria ile.

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 16

Ibara ya 17

Ibara ya 18

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19

**MHE. WILLIAM SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 19 (ii) ile Ibara ndogo zaidi (e) nilipendekeza kwamba kama wanatumia “*prescribing anything which anything...*” basi iwe *needs* badala ya *need to be*.

*(Ibara Iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo Juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya UNESCO wa Mwaka 2008**  
*(The UNESCO National Commission Bil, 2008)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Kuundwa kwa Tume ya Taifa ya UNESCO *(The UNESCO National Commission Bill, 2008)* na kuukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa. Naomba sasa Muswada huu ukubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umepita na kilichobaki ni sainei ya Rais. Nawashukuru sana. Kama nilivyosema katika Bunge, ukizunguza

kwenye kiti chako unachangia. Kuchangia kwako hakutufanyi sisi tuseme wewe umesema nini. Kwa hiyo, unapofika tunatoa hoja, tunazingatia hoja yako ile na kuamua, hayo ndiyo maamuzi ya Bunge. Lakini kuchangia hata ukisema sana hiyo bado hujasema. Ndiyo maana waliochangia hao wote walipokuja kwenye kifungu wote tumezingatia kile walichokuwa wanasema na kukubaliana na kuafiki. Hivyo ndivyo tunavyotunga sheria.

Unaweza ukasema sana hata ukalia machozi kama huji na hoja rasmi kwamba mimi nataka wote tuzingatie lile, hujasema, na utakuwa umesema kwa furaha yako! Ndiyo maana unakuta Mheshimiwa Shellukindo na wengine wamesema lakini kama wasingekuja kusema tena hapa tulikuwa na hiari ya kuchukua au kutokuchukua. Kama *you are serious* basi tuambie kwamba *this is what you want*. Kwa hiyo, huo ndiyo utaratibu ambao unafanyika katika kutunga sheria. Maneno hayo ndiyo yanaingia kwenye utungaji wa sheria.

Kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwa *fast* na tunawashukuru sana kama mtaandaa semina lakini kinachotokea sasa hivi kwa utaratibu wetu wa kushirikisha *public* inasaidia sana kupanua wigo wa kuelewa Muswada wetu, sio sisi Wabunge lakini na wananchi ambao wanahusika sana kama wadau. Kwa hiyo, huo ni utaratibu, ni mzuri na umo ndani ya Kanuni zetu kwa maana hiyo bado inaendelea kufanyiwa kazi. Kwa mfano, Muswada wa *Social Security*, kuunganisha *social security* kuna vyombo vingi sana, vyote kusema kuwa viwe chini ya chombo kimoja kazi inafanywa na makundi mbalimbali.

Kwa maana hiyo Miswada mingine mpaka Jumamosi ilikuwa haijaiva, tuliokuwa nao ni huu mmoja na kwa hiyo, hatuna kazi nyingine mchana huu. Nawakumbusha tena mwende kwenye maonyesho *Vodacom*, wana maonyesho yao, mna muda wa kutosha. Waheshimiwa Wabunge naliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 6.25 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 15 Aprili, 2008, Saa Tatu Asubuhi)*